

**UHAKIKI WA WAKATI NA UWASILISHAJI USEMI KAMA VIPENGEEVYA
USIMULIZI KATIKA *UTENZI WA NABII ISA*.**

MAKIRI AGNES KWAKA

C50/80438/2015

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili
katika Chuo Kikuu cha Nairobi**

NOVEMBA, 2018

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine.

Agnes Kwaka Makiri

Tarehe

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii tulioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Pro. Kyallo Wadi Wamitila

Tarehe

Dkt. Zaja Omboga

Tarehe

TABARUKU

Kazi hii naitabarukia wazazi wangu wapendwa, babangu Bw. Paul Kwaka Makiri na mamangu Bi. Esther Luvuno Kwaka.

SHUKRANI

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii aliyonijalia na kuniongoza kufikia kiwango hiki cha elimu.

Kwa namna ya pekee shukrani zangu ziwaendee wahadhiri wangu wasimamizi, Prof. Kyalo W. Wamitila na Dkt. Zaja Omboga kwa kukubali kusimamia tasnifu hii, kujitolea na kutumia muda wao mwingi kunishauri na kunielekeza kufanya kazi hii. Mola awalipe juhudi zao.

Nawashukuru wakubwa wangu wa shirika la watawa wa Mt. Yosef wa jimbo kuu la Mombasa kwa kuniruhusu kuendeleza elimu yangu katika kiwango hiki cha uzamili. Bila kumsahau padre Bedford Kimathi aliekuwa chanzo cha wazo hili na kunitia ari ya kuendelea na elimu. Mungu awabariki.

Shukrani zangu za dhati ziwaendee, kwanza kabisa padre Joseph C. Kitheka kwa mchango na msaada wake mkubwa kwa hali namali na kuona kwamba mahitaji yangu yote ya elimu yamepatikana. Aidha kwa kunihimiza na kunitia moyo hasa wakati mambo yaliponiwia magumu na kujihisi kukata tamaa. Pili, Dkt. Moritz Kruger kwa upendo na msaada wake alionipa daima nilipomwendea. Bila kumsahau Dkt. Timothy Arege kwa upendo na utayari wake nilipomwendea kutaka msaada wake. Asanteni sana. Mungu mwenyezi awape mahitaji yao ya roho na mwili, wasipungukiwe. Kadhalika awajalie furaha katika maisha yao. Mola awalipe maradufu.

Nawashukuru pia wote walionisaidia kwa namna moja au nyingine kufikia kiwango hiki cha elimu. Maulana awajalie heri daima.

IKISIRI

Utafiti huu umechunguza usimulizi katika *Utenzi wa Nabii Isa* kwa kutumia nadharia ya naratolojia. Kazi hii ilijibana katika vipengee viwili vya usimulizi – wakati na uwasilishaji usemi. Kimsingi utafiti huu ulipania kuonyesha jinsi wakati unavyobainika katika utenzi na kuangazia suala la mpangilio wa matukio kwa misingi ya mfuatano wa kiwakati au mpangilio mwingine mbadala unaojitokeza katika utenzi hasa wa Nabii Isa. Katika kuwezesha haya utafiti umejaribu kubainisha mbinu za uwasilishaji usemi zilizotumika. Kadhalika kuchanganua muundo na mtindo wa *Utenzi wa Nabii Isa*. Kutokana na utafiti huu tumetambua kwamba vipengee vya usimulizi vina dhima kubwa katika uelewekaji wa hadithi yenyewe na kupitisha ujumbe katika hadithi. Mathalani maudhui katika hadithi. Aidha utafiti umeonyesha kuwa mbinu anuwai za wakati na uwasilishaji usemi zimedhihirika katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Mathalani katika kipengee cha wakati imebainika kuwa mbinu ya analepsia imetumika zaidi kuliko ile ya prolepsia na katika uwasilishaji usemi, mbinu za usemi halisi na mawazo halisi, usemi wa taarifa na mawazo ya taarifa, usemi halisi huru na mawazo halisi huru na usemi wa taarifa huru zimetumika. Mawazo ya taarifa huru ni mbinu ambayo haijadhihirika katika *Utenzi wa Nabii Isa*.

ORODHA YA VIFUPISHO

Bi.	–	Bibi
Bw.	–	Bwana
Dkt.	-	Daktari
K. m	–	Kwa mfano
K. v	–	Kama vile
M.T.H	–	mawazo taarifa huru
N.k	–	Na kadhalika
Prof.	–	profesa
Uk	–	Ukurasa
U.T. H	–	Usemi taarifa huru
TUKI	–	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

YALIYOMO

IKIRARI.....	i
TABARUKU.....	ii
SHUKRANI.....	iii
IKISIRI.....	iv
ORODHA YA VIFUPISHO.....	v
SURA YA KWANZA.....	1
UTANGULIZI.....	1
1.1 USULI WA MADA.....	1
1.2 TATIZO LA UTAFITI.....	3
1.3 MASWALI YA UTAFITI.....	4
1.4 MADHUMUNI YA UTAFITI.....	4
1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII.....	4
1.6 UPEO NA MIPAKA.....	5
1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA.....	5
1.8 MSINGI WA KINADHARIA.....	7
1.8.1 Wakati.....	11
1.8.2 Uwasilishaji wa usemi.....	12
1.9 MBINU ZA UTAFITI.....	14
1.10 HITIMISHO.....	14
SURA YA PILI.....	15
2.0 WAKATI.....	15
2.1 Utangulizi.....	15
2.2 Idadi marudio/Umara.....	15
2.2.1 Usimulizi mosi.....	16
2.2.2 Usimulizi rudufu.....	17
2.2.3 Usimulizi banifu.....	18
2.3 Muda.....	18
2.3.1 Muhtasari.....	19
2.3.2 Udondoshi.....	20
2.3.2.1 Udondoshi bayana.....	21
2.3.2.2 Udondoshi usio wazi au kikomo.....	21

2.3.2.3	Udondoshi batini	22
2.3.2.4	Udondoshi dhahiri	23
2.3.3	Onyesho	23
2.3.4	Mtuo	25
2.4	Mpangilio	27
2.4.1	Analepsia	27
2.4.1.1	Analepsia ya nje.	28
2.4.1.2	Analepsia ya ndani	28
2.4.1.3	Analepsia mseto.....	29
2.4.1.4	Analepsia wasifu	29
2.4.2	Prolepsia	30
2.4.2.1	prolepsia ya ndani.....	31
2.5	Hitimisho	32
	SURA YA TATU	33
	3. 0 UWASILISHAJI USEMI.....	33
	3.1 Utangulizi	33
	3.2 Usemi halisi na mawazo halisi	33
	3.3 Usemi halisi huru na mawazo halisi huru.....	36
	3.4 Usemi wa taarifa na mawazo taarifa.....	38
	3.5 Usemi wa taarifa huru na mawazo taarifa huru	41
	3.6. Hitimisho	43
	SURA YA NNE	45
	4.0 MUUNDO, MTINDO NA MAUDHUI KATIKA <i>UTENZI WA NABII ISA</i>	45
	4.1 UTANGULIZI.....	45
	4.2 MUHTASARI WA KISA CHA NABII ISA	45
	4.3 MAUDHUI KATIKA UTENZI WA NABII ISA	46
4.3.1	Dini	47
4.3.2	Usaliti	50
4.3.3	Dhuluma.	51
4.3.4	Ushujaa	52
4.3.5	Miujiza.....	53
4.3.6	Uvumilivu.....	54

4.3.7 Malezi na maadili	55
4.3.8 Ndoa	56
4.4.1 MUUNDO	56
4.4.1.1 Mizani.....	58
4.4.1.2 Vina	59
4.4.1.3 Mishororo	59
4.4.4 Beti	60
2.4.1.5 Muundo wa utatu.....	60
4.4.2. Mtindo	63
4.4.2.1 Usimulizi	63
4.4.2.2 Lugha.....	66
4.4.2.2.1 Tanakali za sauti	67
4.4.2.2.2 Tashbihi	67
4.4.2.2.3 Takriri	68
4.4.2.2.4 Sitiari	68
4.4.2.2.5 Tabaini.....	69
4.4.2.2.6 Taniaba	69
4.4.2.3 Uhuru wa mtunzi	69
2.5 Hitimisho	70
SURA YA TANO	71
5.0 HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO.....	71
5.1 Utangulizi	71
5.2 Matokeo ya utafiti	71
5.3 Mapendekezo.....	72
MAREJELEO.....	74

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 USULI WA MADA

Wakati na uwasilishaji usemi ni vipengee muhimu katika usimulizi. Usimulizi ni uelezaji wa matukio katika hadithi. Ni muhimu kutambua kwamba hadithi husimuliwa kwa namna mbili kuu. Inaweza kusimuliwa kwa njia ya mdomo au andishi. Katika kuieleza hadithi kwa njia ya uandishi pia kunaweza kuwa matumizi ya nathari kama vile riwaya, tamthilia na hadithi fupi ama kwa ushairi. Hivyo katika uchunguzi wowote wa usimulizi wa hadithi hauna budi njia hizi zizingatiwe. Japo usimulizi umehusishwa sana na maandishi ya kinathari kama vile riwaya, tamthilia, hadithi fupi na novela na hasa zaidi na riwaya, haimaanishi kuwa hizi ndizo tanzu pekee za kifasihi zilizo na usimulizi. Kama tulivyotangulia kusema utanzu wa ushairi pia ni njia mojawapo ya usimulizi. Ukweli ni kwamba ushairi ndio njia kongwe zaidi ya usimulizi. Njia nyingine kama vile drama zilitumia lugha ya kishairi.

Katika usimuliaji wa hadithi au simulizi, kuna vipengee mbalimbali ambavyo huchangia muundo wa hadithi. Muundo huu unapochanganuliwa hufanya hadithi kueleweka na kupata maana yake kwa jumla. Masuala muhimu katika usimulizi kama asemavyo Wamitila (2008: 141) ni, wakati, wakala wa usimulizi, mkabala wa kimtazamo na usemi. Katika kuchanganua vipengee hivi muhimu, basi ni kwamba tunashughulikia swala zima la usimulizi. Kama asemavyo Ong'ondi, (2005) akimnukuu Barry (1995), “usimulizi ni mtalaawa jinsi simulizi huleta maana”

Usimulizi umetokana na au asili yake ni fasihi simulizi na ambayo ndiyo fasihi kongwe. Fasihi simulizi ndiyo iliyoibua fahisi andishi. Kama anavyohoji Mohammed (1995: 82) “Asili ya simulizi ni katika fasihi simulizi ambapo msimulizi yupo mbele ya hadhira hai ambayo inamuona, kumsikiliza na hata kumgusa.” Tofauti na fasihi andishi ambapo msimulizi haonekani, hajulikani, “kiwiliwili cha fanani hakipo, msimulizi hai hayupo, vitendo vyake vya kushughulisha hadhira katika majukwaa havipo.” Mohammed (1995: 83). Katika asili hii ndipo paliibuka kitovu cha utafiti wetu.

Hata hivyo katika ushairi si tungo zote zilizo na usimulizi. Tungo zilizo na usimulizi ni tungo ndefu kama vile tenzi. Ni vyema pia kufahamu kuwa si tenzi zote zinazosimulia hadithi. Kunazo tenzi zilizo na usimulizi na zile zisizo na usimulizi. Mojawapo ya tenzi zisizo na usimulizi ni kama vile *Utenzi wa Mwanakupona* ambao ni wosia wa Mwanakupona kwa bintiye Mwana Heshima akimshauri kuhusu ndoa na kazi za mke nyumbani. Baadhi ya zile zinazosimulia hadithi ni pamoja na *Utenzi wa Tambuka*, *Utenzi wa Fumo Liyongo*, *Utenzi wa Ayub*, *Utenzi wa Siri Li Asirali* na *Utenzi wa Paa na Ngami* miongoni mwa nyingine. Katika tenzi hizi inabainika kwamba kuna zile ambazo zimeangazia vipengee vya wakati na uwasilishaji usemi ambavyo tunataka kuvichambua katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Ni utenzi unaoeleza kisa cha maisha ya Nabii Isa tangu asili yake hadi hatima yake kama tutakavyoona katika uchambuzi wa kazi yenyewe. Zipo tafiti zilizotangulia ambazo zimeshugulikia swala hili la usimulizi. Baadhi yao ni Shitemi (2011), aliangalia aina za wasimulizi, sifa za usimulizi, kuonekana kwa msimulizi, utegemefu wa usimulizi na hadhi ya matazamo katika usimulizi katika *Utenzi wa Siri Li Asirali*. Arege (2012), alichanganua vipengee vya wakati, daraja na sauti na uhusika katika *Utenzi wa Rasi Ighuli* na Kimani (2014), alihakiki arki za usimulizi buni katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayas* miongoni mwa wengine. Katika kazi hizi uchambuzi wa vipengee vya wakati na uwasilishaji usemi katika *Utenzi wa Nabii Isa* havijashughulikiwa. Hivyo kuupa utafiti wetu mwanya wa kiusomi ambao tunadhamiria kuujaza.

Usimulizi unahusu uelezaji wa matukio katika hadithi, ni muhimu basi kuelewa kwanza hadithi ni nini kabla hatujashughulikia uwasilishaji wa hadithi yenyewe. Tunaposhughulikia hadithi vipengee tofauti tofauti hufumbatwa, ambavyo huchangia pakubwa muundo wa hadithi ambao unapochanganuliwa huleta maana katika hadithi na kufanya ieleweke. Hivyo tunapochanganua jinsi vipengee vya usimulizi vinavyochangia kuleta maana katika hadithi tunashughulikia usimulizi. Wamitila, (2003: 54) anaeleza, “hadithi ni mfululizo wa matukio kwa kuzingatia mfuatano au mpangilio wake kiwakati.” Tunakubaliana naye kwamba tunapozungumzia kuhusu hadithi, wakati na mahali ni muhimu pia ziingaziwe kwa sababu matukio hutokea kwa wakati fulani na husimuliwa mahali fulani. Kadhalika matukio huwa na mpangilio fulani. Matukio katika hadithi lazima yawe na mfululizo wa kutokea kwake. Kwa mfano mtoto hutungwa mimba kisha baada ya miezi tisa tumboni huzaliwa kisha akakua kwa hatua hadi utu uzima wake. Haiwezekani mtoto azaliwe kisha baadaye kutungwa

mimba. Yakitokea hivi katika masimulizi basi haitakuwa ni hadithi bali maelezo tu ya namna yake.

Wahusika ni kipengee kingine muhimu katika hadithi, kwani matukio yote katika hadithi hayawezi kutokea bila ya wahusika. Wahusika ndio watendaji wa matukio katika hadithi. Katika hali ya kutenda na kutendeana ndipo hadithi huendelea. Hata hivyo wahusika katika hadithi hawaendelezi hadithi kwa kutenda tu bila mawasiliano. Hivyo ni kwamba uwasilishaji kwa kutumia lugha ni kipengee kingine muhimu katika uendelezaji wa hadithi. Tukiweka mawazo haya pamoja tunakubaliana na mawazo ya Ong'ondi katika tasnifu yake (2015) kuwa hadithi ni masimulizi yanayojengwa kwa matendo na usemi wa wahusika kulingana na jinsi yanavyofuatana kiwakati na kimahali.

Japo tumeeleza kwamba matukio lazima yafuatane kiwakati ndipo kuwe na hadithi, waandishi wamezua mbinu ambayo inapinga jambo hili. Mbinu hii inaleta tukio ambalo hutangulia kutendeka linawekwa mbele na lile lingetokea baadaye kuwekwa mwanzo wa hadithi. Mbinu hii ya kifasihi wataalamu wameita mbinu rejeshi ambayo Wamitila (2003: 117) anaeleza kuwa“ni mbinu anayotumia mwandishi kuyaeleza matukio yaliyotokea wakati wa nyuma ya wakati wa hadithi”

Usimulizi umebeba mambo mengi muhimu, na hatutaweza kuyashughulikia yote. Hii ni kwa sababu ya wakati na pia utafiti hauwezi kushughulikia mambo yote. Hivyo basi utafiti wetu umeteuwa vipengee muhimu viwili vitakavyoshughulikiwa tukijikita katika *Utenzi wa NabiiIsa*, ambavyo ni wakati na uwasilishaji usemi kama ielezavyo mada yenyewe.

1.2 TATIZO LA UTAFITI

Utafiti huu unaangazia suala la usimulizi katika ushairi hasa kwa kuangazia vipengee viwili vya kimsingi–ubainikaji wa wakati na uwasilishaji usemi. Kimsingi utafiti huu unapania kuonyesha jinsi wakati unavyoshughulikiwa kiutunzi na jinsi unavyojibainisha katika utenzi. Vilevile utafiti huu una lenga kuangazia suala la mpangilio wamatukio kwa misingi ya mfuatano wa kiwakati au mpangilio mwingine mbadala unaojitokeza katika utenzi mahususi *Utenzi wa Nabii Isa* wa Musa Mzenga. Katika kuangalia suala la mantiki ya mpangiliowa

matukio, mfuatano wa kiwakati, utafiti huu umejaribu kubainisha mbinu zilizotumikishwa kuwezesha haya – kama vile, mbinu za usemi.

1.3 MASWALI YA UTAFITI

Utafiti huu unalenga kujibu maswali yafuatayo;

- i. ni vipengee vipi vya wakati na uwasilishaji usemi vinavyodhihirika katika *Utenzi wa Nabii Isa?*
- ii. je, vipengee hivi vina dhima gani katika *Utenzi wa Nabii Isa?*
- iii. je, vipengee hivi vina vimechangia vipi uelewekaji wa ujumbe ulio katika hadithi katika *Utenzi wa Nabii Isa?*
- iv. vipengee hivi ninasaidiaje kuibainisha maudhui, muundo na mtindo katika usimulizi wa hadithi ya Nabii Isa katika *Utenzi wa Nabii Isa?*

1.4 MADHUMUNI YA UTAFITI

Utafiti huu umeongozwa na malengo yafuatayo;

- i. kubaini vipengee vya wakati na uwasilishaji usemi katika *Utenzi wa Nabii Isa.*
- ii. kujadili dhima ya vipengee vya usimulizi katika kuwasilisha ujumbe katika *Utenzi wa Nabii Isa.*
- iii. kuchanganua vipengee vya usimulizi katika *Utenzi wa Nabii Isa* ili kuonyesha jinsi vimechangia kuibua maudhuianuwai katika hadithi ya Nabii Isa katika *Utenzi wa Nabii Isa.*
- iv. kubaini muundo na mtindo katika usimulizi wa hadithi ya Nabii Isa katika *Utenzi wa Nabii Isa*

1.5 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Swala la usimulizi limehusishwa na maandishi ya kinathari kama vile riwaya, tamthilia na hadithi fupi na hasa riwaya. Hivyo ni wazi kwamba zipo tafiti nyingi kuhusu usimulizi ambazo zimejikita katika maandishi ya kinathari. Mfano wa watafiti waliotafiti usimulizi na ambao wamejikita katika maandishi ya kinathari ni pamoja na Ong'ondi, aliyehakiki usimulizi katika riwaya ya *Walenisi*, Khamisi alishughulikia usimulizi katika tamthilia ya

Kijiba cha Moyo na Mstahiki Meya miongoni mwa wengine. Hivyo utafiti huu unatumainiwa kutoa nyongeza kwa kile ambacho kishatafitiwa. Sababu ni kwamba utafiti hauwezi kushughulikia mambo yote, hutegemea mhakiki anataka kutafiti nini.

Kwa kuchambua *Utenzi wa Nabii Isa*, utafiti huu unatoa mchango maalum kwa wasomi na waandishi kwa jinsi tulivyoshughulikia vipengee teule vya utafiti huu ambavyo havijahakikiwa na wasomi wengine waliotangulia kutafiti utenzi huu. Kwa mfano Owallah, (2013) katika tasnifu yake ya uzamili alihakiki maudhui teule katika *Utenzi wa Nabii Isa* na Abdallah (1976) alihariri *Utenzi wa Nabii Isa*. Mbali na kutoa mchango wa kiusomi, twatumai baada ya kusomwa na kueleweka, utafiti huu utakuwa chachu ya kuamsha ari za wasomi wengine kufanya tafiti nyingine zinazohusu utenzi wa Nabii Isa katika vipengee tofauti tofauti vya fasihi.

1.6 UPEO NA MIPAKA.

Utafiti huu umechunguza *Utenzi wa Nabii Isa* (1977) wa Musa Mzenga ulio na beti 834. Kwa sababu ni vigumu kuzungumzia kuhusu suala zima la usimulizi, utafiti huu umejikita katika vipengee viwili vya usimulizi – wakati na uwasilishaji usemi. Vipengee ambavyo havitashughulikiwa katika utafiti huu ni mtazamo wa usimulizi, viwango na sauti za usimulizi, na uhusika na wahusika. Utafiti huu pia umedhamiria kujadili muundo na mtindo katika utenzi huu. Maudhui pia hayakuachwa nyuma, yamejadiliwa kadiri yanavyoibuliwa na mada husika. Aidha utenzi wenyewe utaelezwa kwa muhtasari ili kupata msingi wa hadithi hii ya Nabii Isa.

Nadharia inayoongoza utafiti huu – naratolojia ikizingatia vipengee viwili vya usimulizi ambavyo ni wakati na uwasilishaji usemi imejadiliwa. Vitabu vya wataalamu mbalimbali wa nadharia iliyopendekezwa vimesomwa na kujadiliwa kwa kina. Aidha majarida ya kiusomi na vile vile tasnifu za watafiti wengine zimesomwa ili kupata ufahamu zaidi, mawazo na mwelekeo wa kufafanua mada ya utafiti huu.

1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Katika sehemu hii tumeangazia baadhi ya wasomi tahakiki ambazo zinapatikana kuhusiana na mada yetu. Ong'ondi, (2005) katika tasnifu yake alihakiki usimulizi katika riwaya ya

Walenisi ya Katama Mkangi. Katika uhakiki wake, alijikita katika vipengee mbali mbali vya usimulizi vikiwemo, wakati, mtazamo kwa kuangalia tofauti zilizopo kati ya usimulizi na mtazamo. Alichambua pia sawia za usimulizi zilizopo katika riwaya hii ya *Walenisi* na kuonyesha aina za usimulizi na jinsi zinavyodhihirika. Aidha unenaji na fikira zimejadiliwa katika tasnifu hii ya Ong'ondi. Tofauti na Ong'ondi, utafiti wetu tumehakiki usimulizi kwa kujikita katika vipengee viwili, wakati na uwasilishaji usemi, uwanja wetu wa utafiti ukiwa *Utenzi wa Nabii Isa*. Hata hivyo utafiti wa Ong'ondi umetufaa katika kuchambua uwasilishaji usemi ambao yeye ameuita unenaji, nakatika kuchambua kipengee cha wakati ambavyo ni vipengee vya usimulizi vilivyoteuliwa katika kazi hii yetu.

Mulama, (2011) amechunguza usimulizi katika *Utenzi wa Siri Li Asirali* akitumia nadharia ya naratolojia. Katika uchanganuzi wake wa usimulizi alijikita katika vipengee vifuatavyo; aina ya wasimulizi, sifa za usimulizi, kuonekana kwa usimulizi, utegemefu wa usimulizi na hadhi ya mtazamo katika usimulizi. Aidha mtazamo wa ndani na wa nje pia imechunguzwa pamoja na sawia za mtazamo. Kipengee cha wakati hakikubakishwa kwani ni kipengee muhimu katika usimulizi. Utafiti huu umetupa mwelekeo wa kipengee cha wakati. Japo utafiti wetu unajikita katika kuhakiki usimulizi katika *Utenzi wa Nabii Isa*, utafiti huu umetufaa kwa kutupa mawazo kuhusu kipengee cha wakati.

Arege,(2012) katika tasnifu yake ya uzamifu, alihakiki vipengee vya usimulizi vya wakati, ngazi na sauti za usimulizi na uhusika na wahusika katika *Utenzi wa Rasi 'Ighuli*. Kadhalika alitumia nadharia ya naratolojia kuhakiki kazi yake. Arege hakuhakiki kipengee cha uwasilishaji usemi. Kwa sababu hii kuacha pengo la uhakiki wa kipengee hiki. Hivyo basi utafiti huu umedhamiria kuhakiki kipengee cha uwasilishaji usemi pamoja na wakati katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Hata hivyo japo kuna tofauti ya utafiti wa Arege na utafiti huu, mawazo yake yametusaia kuelewa nadharia tuliyoteuwa, kutupa mwelekeo na namna ya kukabili mada yetu.

Ouma, (2013) amechunguza uhakiki wa maudhui katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Nadharia aliyotumia ni ile ya uyaakinifu katika jamii. Sawia na Ouma utafiti wetu umeteua *Utenzi wa Nabii Isa* kama uwanja wa utafiti. Tofauti kati yetu na Ouma ni kwamba sisi tutachambua hadithi iliyomo katika utenzi huu jinsi ilivyosimuliwa kwa kuchunguza vipengee vya

usimulizi. Hata hivyo maelezo ya Ouma yametusaikia katika kuelewa vema hadithi ya Nabii Isa katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Hivyo kutupa mwelekeo na namna ya kuchambua kazi yetu ambapo *Utenzi wa Nabii Isa* ndio kiini cha kazi hii yote.

Kimani (2014) katika utafiti wake wa uzamili alitafiti arki za usimulizi bunilizi katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*. Katika utafiti wake alijikita katika kipengee cha usimulizi, mpangilio wa matukio na mtazamo wa usemi. Tofauti na Kimani utafiti wetu umejadili kipengee cha wakati na cha uwasilishaji usemi kwa kujifunga katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Utafiti huu umetufaa katika kutuelekeza katika mpangilio wa matukio ambao ni mojawapo ya kipengee cha wakati.

Zipa kazi nyingi ambazo zimechunguza jambo hili la usimulizi wa hadithi. Nyingi zikijikita katika maandishi ya kinathari. Tulizotaja hapo juu ni miongoni mwa nyingi ambazo hatuwezi kuzitaja zote. Hata hivyo tunaamini zina msaada mkubwa kwa utafiti huu kwani zimetuelekeza na kutupa mwanga katika kujadili mada yetu na pia tumezirejelea mara kwa mara kila tunapochambua mada yetu. Aidha tumegudia kwamba *Utenzi wa Nabii Isa* bado haujapata umaarufu. Hivyo tunatumai kwamba utafiti wetu umetoa mchango mkubwa katika fasihi.

1.8 MSINGI WA KINADHARIA

Utafiti huu umeelekezwa na nadharia ya naratolojia. Naratolojia, kama asemavyo Barry (2002: 222-223) ni taalumainayochunguza jinsi simulizi zinavyojenga maana pamoja na mbinu zote zinazotumika katika usimulizi wa hadithi. Cha muhimu katika naratolojia si kusema na kufasiri hadithi bali kuchunguzaasiliya hadithi na kufafanua elementi mbalimbali katika hadithi. Naratolojia inahusika pia simulizi. Wamitila, (2002) akimnukuu Prince, anaeleza, “simulizi ni uelezaji wa tukio moja au mengi ya kihalisia au kibunilizi... tokeo na njia, lengo na tendo, muundo na uundaji (wake).”

Anaendelea kueleza simulizi kwa kumnukuu pia Genette akisema kuwa dhana hii inaweza kuelezwa vyema kwa kurejelea mambo matatu tofauti ambayo ni, kueleza kauli ya kisimulizi au kimaandishi au isiyo ya kimaandishi, mfuatano wa matukio halisi au kibunilizi au yanayolengwa na usemi fulani na kueleza tendo lenyewe la kisimulizi au usimulizi. Mambo haya anayaita simulizi, hadithi na usimuliaji mtawalia. Mambo haya matatu ni muhimu sana

katika usimulizi, hivi kwamba yakikosekana basi usimulizi hautokuwepo isipokuwa maelezo tu.

Onega na Landa (1996: 12) wanaeleza kuwa naratolojia ni sayansi ya usimulizi. Wanadai kwamba dhana hii ilipewa umaarufu miaka ya sabini (1970) na wanamuundo kama vile Genette. Mmoja wa wananaratolojia mashuhuri ni Gerard Genette. Genette hatazami hadithi tu, bali jinsi hadithi inavyosimuliwa, ni nini kinachosimuliwa na mchakato wa kuisimulia hadithi yenyewe. Genette (1980: 25 - 26) katika kitabu chake *Narrative Discourse* anaeleza maana tatu za simulizi, ya kwanza anasema simulizi ni kauli. Ama ya kutamkwa kwa mdomo au ya kimaandishi inayothibitisha usemi wa tukio au matukio. Maana ya pili ni kuwa simulizi ni mfuatano wa matukio halisi au ya kubuni. Na maana ya tatu anasema kuwa simulizi ni tukio linalotegemea mtu kuhadithia au kusimulia jambo. Genette anaendelea kueleza kuwa uwasilishaji wa usemi unatokana na kitendo cha kuongea. Hivyo basi bila usimulizi hakuna kauli na hata wakati mwingine kukosekana maudhui ya simulizi. Anaendelea kueleza kwamba simulizi linaweza kuwa kimimesia, yaani simulizi au hadithi inaweza kuwasilishwa kwa namna ya onyesho kama katika drama kwa kutumia dayalojia ambapo yanayosemwa na kutendwa yanawekwa wazi mbele ya msomaji na kumfanya ahisi kwamba anayaona na kuyasikia mambo hayo, au kwa njia ya daigesia. Yaani kwa njia ya kueleza bila kujenga maono kwa msomaji kwamba yanayosemwa na kutendeka anayaona mbele yake.

Genette anaeleza jinsi hadithi inavyosimuliwa kwa kuangalia mpangilio wa matukio kiwakati. Kwamba matukio katika hadithi yanaweza kuelezwa kwa kufuatana jinsi yanavyotokea au kusimuliwa kwa kuweka matukio yaliyotangulia mbele. Hali hii ya kusimulia matukio yaliyopita au kutangulia anaitwa analepsia (mbinu rejeshi) au kwa kusimulia matukio ya nyuma kwanza. Mbinu inayoitwa prolepsia (mbinu elekezi). Kadhalika Genette anaeleza wahusika wanavyotoa ujumbe au jinsi lugha inavyotumika. Hivi ni kusema kwamba maneno na mawazo ya wahusika yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya usemi au mawazo halisi au kwa njia ya usemi au mawazo ya taarifa.

Wolf, (2002) anaigawa naratolojia au simulizi mara tatu; simulizi ya kwanza ambayo anasema kuwa linajumlisha baadhi ya yaliyomo na matokeo katika hadithi, simulizi ya pili, inahusu jambo la kidhahania, hivyo inamaanisha ni hadithi yenyewe ambayo inaweza

kusimuliwa kwa njia tofauti tofauti mathalani tenzi, drama, filamu n.k. Nayo simulizi ya tatu ni muungano wa simulizi ya kwanza na ya pili ambazo zinadhihirika katika njia mahususi. (ambayo si mdomo pekee inayosimuliwa na msimulizi lakini kazi yenyewe au nakala) kama vile michezo ya kuigiza na sanaa za maonyesho miongoni mwa nyingine.

Kwa kutumia mawazo ya Wananaratolojia hawatunabaini kuwa naratolojia ni kazi yenyewe ya fasihi aidha andishi au simulizi inayoweza kuwasilishwa kwa njia tofauti tofauti mathalani, hadithi fupi , drama, riwaya, novella, tenzi n.k wahakiki wanakubaliana kuwa simulizi haina budi kuhusisha usimuliaji wa tukio au matukio. Ikiwa sifa hii itakosekana, simulizi husika itabaki kuwa maelezo tu.

Prince, (1982: 5) akimnukuu Ronald Barthes katika kitabu, *An Introduction to The Structural Analysis of Narratives*, anasema kuwa ziko aina nyingi za simulizi na tanzu nyingi tofautitofauti ambazo zimegawanyika katika njia tofauti za uwasilishaji. Kati ya njia hizi ni kuongea kwa ufasaha aidha katika maandishi au kwa mdomo, picha, ishara n.k. anasema kuwa simulizi ziko katika visasili, ngano, hekaya, hadithi fupi, tenzi, tanzia, filamu na njia nyingine za kuwasilisha ujumbe, na katika haya yote ziko kila wakati, kila mahali na katika kila jamii na kwamba hakuna na hakutakuwa na jamii yoyote isiyokuwa na simulizi, kila jamii na aina ya tamaduni ina simulizi zake ambazo hufurahiwa na watu hata wa asili tofauti. Hivyo basi Prince anaeleza simulizi kuwa ni uwasilishaji wa matukio halisi au ya kibunilizi na hali katika mfuatano wa kiwakati. (uk. 1).

Prince, (1982: 5) anaeleza naratolojia kuwa ni stadi ya aina na utendaji kazi wa simulizi. Anasema pia kuwa naratolojia inachunguza yale yote ambayo yanafanana katika simulizi na tofauti zake, haijishughulishi na historia ya thamani ya ujumi bali na sifa zinazobainisha simulizi na mifumo mingine muhimu na mitindo ya sifa hizi. Kimsingi, jukumu lake ni uchanganuzi wa undani wa vifaa vinavyoongoza kikamilifu maelezo ya simulizi naufahamu wa utendaji kazi wake.

Katika simulizi, mambo matatu lazima yawepo. La kwanza ni yule anayesimulia au msimulizi. Prince anaitanafsi ya kwanza “mimi.” Jambo la pili ni hadhira au yule anayesimuliwa, ambaye Prince pia anamwita mtu katika nafsi ya pili “wewe” na jambo la

tatu ni kile kinachosimuliwa, ambaye pia anamwita mtu katika nafsi ya tatu, “yeye.” Mambo haya yanatuelekeza kwa uwasilishaji wa usemi. Hivyo tutajadili uwasilishaji huu katika sehemu inayofuata ya uwasilishaji wa usemi hapo chini.

Landa, (1990) katika kitabu chake, *Narrative Theory*, amejadili vipengee vingi vya naratolojia akijikita katika mawazo ya wanaratolojia tofautitofauti, baadhi yaoni Tomashevsky, Bal na Genette. Baadhi ya dhana ambazo amezijadili ni pamoja na ploti, uhusika, ubunifu, wakati, mtazamo, taswira, uwasilishaji wa usemi n.k. Hatujajadili dhana hizi zote, tumeangazia tu dhana zinazohusika na utafiti huu ambazo ni wakati na uwasilishaji wa usemi.

Katika uwasilishaji wa usemi Landa (ameshatajwa) amechambua vipengee vifuatavyo, msimulizi na nafasi ya masimulizi, aina za nafasi za masimulizi n.k. Katika simulizi Landa anaeleza kuwa simulizi ni ishara zinazowasilishwa kwa mfuatano wa matukio. Anaendelea kueleza kuwa uwasilishaji wa ishara hizi ni kazi ya wakala, na msimulizi hapa ndiye wakala ambaye anaeleza wazi simulizi au hadithi. Landa analeta dhana ya msimulizi na msimuliwa au anayesimuliwa. Katika nafsi ya kwanza “mimi” inamaanisha kuwa msimulizi, ambaye ndiye nguli wa tendo au tukio linalowasilishwa. Nafsi ya pili “wewe” huwasilishwa tofauti na “Yeye” anahusishwa na kutokuwepo kwao katika hali ya usemi. Hili ni dhihirisho kuwa, kama tulivyo na viwakilishi nomino katika nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu, vivyo hivyo katika kazi ya fasihi kuna nafsi hizi tatu.

Katika kipengee cha wakati Landa anaeleza kuwa, kama kazi nyingine za fasihi, lugha pia hujidhihirisha kiwakati. Kuhusu dhana hii Landa anaeleza kuwa kuna wakati bunifu (fabula time) na wakati uwasilisho (presentation time). Anaeleza kuwa nyakati hizi mbili zimeachana kwa nafasi ndogo sana na wakati mwingine huingiliana. Hivyo badala ya kuwa na aina mbili za wakati tunakuwa na aina moja ambayo ni wakati-matini na aina nyingine anayoeleza pia ni wakati-hadidhi. Anasema kuwa wakati hadithi hutokea katika uhusiano au mwingiliano baina ya wakati bunifu na matini. Ameendelea kugawa wakati katika sehemu nyingine kama vile; muda, mpangilio, idadi marudio n. k uchambuzi huu wa Landa pia ni muhimu kwetu kwani umetufaa kutupa mawazo ya kuchambua vipengee vilivyoteuliwa kutatua swala letu la utafiti.

1.8.1 Wakati

Wakati ni kipengee cha naratolojia ambacho kimejadiliwa, kuchunguzwa na kushughulikiwa na wananaratolojia na watafiti wengi wakiwemo, Genette, Bal, Rimmon-Kenan miongoni mwa wengine. Kipengee cha wakati ni muhimu sana kwa sababu matukio yoyote yale hutendeka katika wakati maalum. Kwamba tukio hili hutanguliwa na hili au tukio hili hutokea baada ya hili. Kwa mfano katika hali halisi binadamu kabla ya kuzaliwa hutungiwa mimba kwanza, kisha azaliwe na kukua pole pole hadi utu uzima wake au hatima yake. Hivyo wakati ni kipengee kinachohusika na jinsi wakati unavyoshughulikiwa katika hadithi. Ni kipengee kinachohusika na jinsi wakati unavyoshughulikiwa katika hadithi.

Genette (1980: 33), anaeleza kuwa wakati-hadithi uko mara mbili, kuna wakati wa kile kinachosimuliwa na Wakati wa simulizi. Uwili huu wa wakati ndio unaojulikana kama wakati-hadithi na wakati-matini mtawalia. Ili kuchanganua wakati vyema, Genette anasema, lazima vigezo vitatu viangaliwe. Vipengee hivi ni mpangilio wa mfuatano wa matukio katika hadithi na mpangilio wake (matukio) katika simulizi, mwingiliano wa muda wa matukio katika sehemu za hadithi na urudiaji ambao ni uhusiano wa urudiaji kati ya matukio ya hadithi na yale ya simulizi. (uk. 35). Kwa muhtasari wakati katika usimulizi umegawika katika vigezo vitatu vilivyo na uhusiano mkubwa, ambavyo ni mpangilio, muda na idadimarudio.

Rimmon - Kenan (2002: 44) anaeleza wakati kuwa ni mpangilio wa matukio katika hadithi. Naye Wamitila (2003: 348) anasema kuwa wakati ni dhana katika fasihi inayotumiwa kueleza vipindi ambapo hali na matukio yanasimuliwa na uwasilishaji wake hutokea. Aidha hutumika kurejelea kipindi cha kihistoria ambacho ni msingi mkuu wa kazi husika. Kama dhana nyingine zozote wakati unaweza kuwakilishwa na matini ya usimulizi. Pia wakati sio tu dhamira inayorudiwarudiwa katika simulizi bali mojawapo ya kiambajengo cha hadithi na matini. Hivyo wakati, katika simulizi unaweza kuelezwa kama uhusiano uliopo wa utaratibu wa matokeo baina ya hadithi na matini. Kama Genette, Rimmon-Kenan anazua dhana mbili za wakati; wakati- hadithi na wakati-matini.

Wamitila (2003: 348), anaeleza wakati-hadithi kuwa ni dhana inayorejelea wakati unaochukuliwa na hadithi fulani kutoka mwanzo hadi mwisho. Unaweza kuwa siku chache,

miezi na hata miaka kadhaa. Nao wakati matini ni wakati unaochukuliwa na msomaji fulani kuisoma hadithi. Dhana hii hutofautiana kati ya msomaji mmoja na mwingine kwa sababu kasi zao za usomaji hutofautiana, hauna njia ya kuutathmini.

Pia wakati sio tu dhamira inayorudiwarudiwa katika simulizi bali mojawapo ya kiambajengo cha hadithi na matini. Hivyo wakati, katika simulizi unaweza kuelezwa kama uhusiano uliopo wa utaratibu wa matokeo baina ya hadithi na matini. Jambo hili linazua dhana mbili za wakati; wakati hadithi na wakati matini. Kipengee cha wakati kinaweza kuangaliwa kwa kuvichunguza vigezo vingine ambavyo ni, mpangilio, muda, na idadimarudio. Mambo haya yatajadiliwa kwa kina katika kazi yenyewe ya stadi hii.

1.8.2 Uwasilishaji usemi

Uwasilishaji usemi hutumiwa kueleza namna ambavyo maana hutolewa kwa kutumia lugha. Dhana ya uwasilishaji usemi inahusishwa na mwanafalsafa Plato. Genette, (1980: 162) na Rimmon-Kenan, (2002: 107) wakimnukuu Plato katika kitabu chake *The Republic* juzuu ya 3 wanaeleza kuwa kuna aina mbili za kusimulia hadithi - ama katika usemi halisi au usemi wa taarifa. Njia hizi wanaziita diegesia na mimesia mtawalia. Wanaeleza kuwa katika diegesia sifa kuu ni ile ya kuwa mshairi mwenyewe ndiye msemaji na anajitoa waziwazi na anaweza kutambulika. K. m katika utenzi huu wa Nabii Isa, Musa Mzenga ambaye ndiye mshairi pia ndiye msemaji. (ubeti 1 – 41). Kwa upande mwingine, mimesia sifa yake kuu ni kwamba mtunzi au mshairi hajitokezi waziwazi kama ndiye msemaji. Amejificha. K. m

“Maria yupo?”

“hayupo.”

“kaendapi?”

“sokoni.”

Katika daraja hizi mbili kuu za uwasilishaji usemi (diegesia na mimesia), ziko mbinu tofauti tofauti za kuwasilisha usemi katika kazi ya fasihi. Wamitila (2008: 97) ameorodhesha mbinu nane ambazo ni: usemi halisi, mtindo/mawazo halisi, usemi wa taarifa, mawazo/mtindo ya taarifa, usemi halisi huru, mawazo halisi huru, usemi wa taarifa huru na mawazo ya taarifa huru. Baadhi ya mbinu hizi (hasa zinazojitokeza katika utungo) zitachambuliwa kwa kina katika kazi yenyewe ya utafiti huu ambayo ni mojawapo ya malengo ya kazi hii.

Genette, (1980: 171 - 2) anaeleza kwamba katika stadi yoyote ya usemi katika simulizi lazima kuchanganua pia umbali uliopo baina ya msimulizi na hadithi. Kwamba umbali huu husaidia katika kuamua ni mbinu gani sahihi ya kupitisha ujumbe katika simulizi, aidha inasimulia matendo ya mhusika au inasimulia maneno ya mhusika. Genette ameorodhesha mbinu nne za kuwasilisha usemi mbazo ni, usemi halisi, usemi halisi huru, usemi taarifa na usemi taarifa huru.

Prince (1982: 47) anaweka mambo matatu muhimu katika usimulizi, na kwamba mambo haya yanarejelea uwasilishaji wa usemi katika simulizi. Prince anaeleza kuwa msimulizi anaweza kutoa taarifa kuwa mhusika amejieleza kwa maneno na badala yake akahusisha vitendo vya matukio yake kama matukio yasiyo ya vitendo (vitendo katika fikira). K. m nitaenda huko saa kumi na moja kumtembelea. Pia uwasilishaji unaweza kuwa wa maneno au usio wa maneno. Lakini msimulizi anaweza kuwasilisha matukio kimatendo na pia kuwasilisha maneno ya mhusika kwa njia wazi au isiyo wazi. K. m

- i. Nitaenda huko saa kumi na moja kumtembelea
- ii. Alisema (akijisemea); “nitaenda huko saa kumi na moja kumtembelea.
- iii. Ataenda huko saa kumi na moja kumtembelea.
- iv. Alisema, (akijiambia) kwamba ataenda huko saa kumi na moja kumtembelea.

Katika sentensi ya kwanza, anaita usemi huu, usemi halisi huru, sentensi ya pili ni usemi halisi, sentensi ya tatu ni usemi taarifa huru, nayo ya nne ni usemi taarifa (uk. 47). Kama Genette, Prince anatupa aina nne za uwasilishaji usemi, ambazo ni pamoja na, usemi halisi, usemi halisi huru, usemi wa taarifa na usemi wa taarifa huru. Prince anaendelea anaeleza kwamba, tofauti inaweza kutokea katika aina ya usemi ya kwanza hivi kwamba, mhusika anaweza kutamka sentensi au aziunde tu katika fikira zake bila kuzitamka. Katika hali hizi mbili, Prince anaita ile ya kuzitamka, monolojia ya ndani. Pia katika usemi halisi huru mhusika anaweza kuwasilisha mawazo yake kwa njia ya lugha ambayo haiheshimu kanuni za mofolojia na sintaksia. K.m kukosa sarufi, kukosa uakifishaji, sentensi fupifupi zisizokamilifu n.k.

1.9 MBINU ZA UTAFITI

Utafiti wetu umejikita katika fasihi. Kwa hivyo umefanyika maktabani wala si nyanjani. Data iliyotumiwa katika utafiti huu ni nyaraka msingi ambayo ni *Utenzi wa Nabii Isa*. Katika data msingi tumejishughulisha na wakati na uwasilishaji usemi. Nyaraka Fuatizi zilizotumika ni majarida na vitabu. Data hii imekusanywa kwa kusoma matini zilizochapishwa kuhusiana na mada teule ya utafiti huu pamoja na zile zinazohusu nadharia ya naratolojia ambayo imeteuliwa kuongoza utafiti huumbali na matini zilizochapwa, tumesoma pia tasnifu zinazohusiana na kazi hii. Tafiti hizi zimetusaia kupata pengo na kutoa maelezo na maelekezo mengine ya jinsi ya kufanya utafiti huu. Aidha mtandao umetumika kwa kutupa vitabu vya wataalamu kuhusu nadharia iliyoteuliwa, tasnifu za watafiti wengine na majarida yaloyotunika.

Utenzi wa Nabii Isa ambao ndio utenzi ulioteuliwa kufanyia utafiti huu ulichaguliwa kimakusudi. Utenzi huu umesomwa kwa kina na kwa maakini ili kupata vipengee vya usimulizi ambavyo vimejadiliwa katika utafiti huu. Zana zilizotumika katika ukusanyaji data ni pamoja na kalamu na karatasi kunakili mambo muhimu yanayohusaina na mada ya utafiti wakati tulipokuwa tukisoma nyaraka mbalimbali.

1.10 HITIMISHO

Katika sura hii tumetoa mambo ambayo ni ya kiutangulizi ya utafiti huu. k.v. usuli wa mada, swala la utafiti, maswali ya utafiti, madhumuni, upeo na mipaka, sababu za kuchaguwa mada na yaliyoandikwa kuhusu mada. Aidha msingi wa nadharia umejadiliwa. Vigezo vya wakati na uwasilishaji usemi vimejadiliwa kwa kina katika kazi yenyewe katika sura ya pilina tatu. Katika sura ya nne, maudhui, muundo na mtindo zimejadiliwa.

SURA YA PILI

WAKATI

2.1 Utangulizi

Katika sura hii tumechanganua wakati ambao ni mojawapo ya vipengee muhimu vya usimulizi. Jambo hili litapata uwanja katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Ni katika wakati ambamo tumepatawahusika na matukio. Katika kuchanganua wakati mambo matatu huhusika au kuchunguzwa. Nayo ni, muda, idadi marudio na mpangilio. Aidha wakati hadithi na wakati matini zimeshughulikiwa. Wakati hadithi hurejelea wakati unaochukua hadithi kutoka mwanzo hadi mwisho. Unaweza kuwa siku moja, mwaka mmoja au hata karne na zaidi. Kwa upande mwingine, wakati-matini ni wakatiaonaoweza kuchukua msomaji kuisoma matini. Kuna shida ya kutathmini wakati-matini tukifahamu kwamba kila msomaji ana kasi yake ya kusoma na hivyo kutofautiana katika muda mtu anaochukua kusoma matini ile ile moja. Kazi hii basi imeshughulikia jinsi wakati unavyodhihirika katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Ni sawa kusema kuwa wakati ni kipengee muhimu katika hadithi. Kwa hivyo inahalisi kusema kuwa wakati katika simulizi ni uhusiano kati ya hadithi na matini. Yaani uhusiano wa kiutendekaji wa matukio kimfuatano.

2.2 Idadi marudio/Umara

Dhana hii inarejelea ni mara ngapi tukio limetokea katika hadithi na katika matini yenyewe. Kwamba katika kutendeka tukio linaweza kutendeka au linaweza kupatikana katika matini mara kadhaa. Umara ni mojawapo ya kipengee kikuu katika muda wakati. Kama asemavyo Genette, (1980: 113)

Idadi marudio ni mahusiano kati ya simulizi na diagesia.
Tukio haliwezi kutendeka tu, bali pia linaweza kutendeka
tena na tena, au kurudiwa. Aidha kauli ya kisimulizi haiwezi
kutolewa tu bali pia kutolewa au kuandikwa tena na tena au
kurudiwa maranyingi katika matini hiyo hiyo.

Wamitila, (2002: 144) anakubaliana na Genette kwamba idadi marudio ambayo yeye aliita umara ni dhana inayorejelea mara ambazo matukio hutokea katika hadithi na mara ngapi matukio hayo yanasimuliwa. Sawia na Genette, Wamitila ameanisha aina tatu za idadi marudio, kwamba tukio lililotokea mara moja linaweza kusimuliwa mara moja (Usimulizi

Mosi). Pili, tukio lililotokea mara moja linaweza kusimuliwa mara kadhaa (Usimulizi rudufu) na mwisho, tukio lililotokea mara kadhaa linaweza kusimuliwa mara moja (Usimulizi banifu).

2.2.1 Usimulizi mosi

Aina hii ya umara hutokea pale ambapo tukio limetokea maramoja na kusimuliwa mara moja tu katika hadithi na pia katika matini kuonekana mara moja tu. Aina hii ya usimulizi umesheheni katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Maonyesho mengi yamechukua mkondo huu wa usimulizi. Kwa mfano kuzaliwa kwa Bi. Maryamu binti Imrani (ubeti 37 - 40),

37. Nadhiri yake hakika,
Yote ikakubalika,
Naye akafurahika,
Mimba ilipotukia.

38. Kwa nia ya utakato,
Akashukuria pato,
Asiuone uzito,
Mimba na wake udhia.

39. Endapo yu furahani,
Kubwa isiyo kifani,
Hadi ilipoyakini,
Siku ya kujizalia

40. Ingawa motto wake,
Alovyaa ni wa kike,
Pasi asibadilike,
Huzuni kumjilia.

Matukio mengine ni pamoja na kuzaliwa kwa Nabii Isa (ubeti 177 - 190), ishara iliyotokea baharini na ambayo ilimpa Mtume Zakaria wadhifa wa kumlea Bi. Maryamu binti Imrani (ubeti 78 - 83), mtende uliokuwa hauna hata maua kutoa tende ambazo Bi. Maryamu alikula baada ya kuzaa (ubeti 206 - 213) na kadhalika. Haya yote ni matukio yaliyotokea mara moja na kusimuliwa mara moja.

2.2.2 Usimulizi rudufu

Huu ni usimulizi wa tukio lililotokea mara moja lakini linasimuliwa mara kadhaa katika matini. Kwa mfano kufananishwa kwa sura ya Nabii Isa na yule mfuasi aliyemsaliti kumetokea katika beti zifuatazo;

795. Ndipo mwenye kuongoza,
Vitimbi kuvitimiza,
Mungu akageuza,
Sura kama Masihia.

796. Fatani pasi na shaka,
Haoni kushabihika,
Sura zake kageuka,
Kama za Isa Nabia.

809. Ni huyo salata wenu,
Mulomuhonga kwa tunu,
Meshabihishiwa kwenu,
Mudhani ni Masihia.

818. Yule aloshabihiwa,
Sura za Isa akawa,
Baada ya kuuawa,
Yuli wapi Masihia?

Matukio mengine yaliyotokea mara moja na kusimuliwa mara kadhaa ni kama vile, kuzaa kwa Bi. Maryamu bila kuonana na mume. Jambo ambalo lilifanyika mara moja lakini limetajwa au kusimiliwa mara kadhaa. Kwanza Maryamu anapokutana na mjumbe wa Mungu na kuelezwa kuwa atapata mimba bila ya kuonana na mume au kuolewa (ubeti wa 137 - 142), jambo hili linasimuliwa tena baada ya kuzaa Nabii Isa, Maryamu akiwa na hofu ya jinsi watu watakavyomchukulia kwa kuwa amezaa mwana pasi kuonana na mume mume kimwili. (ubeti 192), pia wakati Bi. Maryamu aliporudi nyumbani jamaa zake walirudia jambo hili kwa kumuuliza ni vipi alipata mwana bila kuolewa au kuwa na mume (ubeti 250 - 251).

2.2.3 Usimulizi banifu

Genette (1980: 115 - 117) anaeleza kwamba usimulizi banifu hutokea pale ambapo tukio linalotokea mara kadhaa linasimuliwa mara moja katika matini. Katika *Utenzi wa Nabii Isa* usimulizi huu unaonekana sehamu nyingi. Kwa mfano, mahudhurio ya Nabii Isa katika ibada na swala msikitini akiwa bado mdogo, chini ya malezi ya malezi ya mama yake Bi. Maryamu (ubeti 290)

Saumu akijali,
Na swala kuikabili,
Siku zote huwasili,
Vipindi vikiwadia.

Maneno “siku zote” yanaashiria hali ya kwenda katika swala bila kukosa au kila mara muda wa vipindi vya swala ufikapo. Pia usimulizi huu umejitokeza katika ziara alizozifanya Nabii Isa wakati akihubiri.(ubeti 338 - 339).

338 Yuli hapati makini,
Si mkaaji nyumbani,
Kukicha yu ziarani,
Miji kuizungukia.

339 Si usiku si mchana,
Hana pa kutulizana,
Kila mji wamuona,
Enda akihubiri.

Katika beti hizi mbili maneno “kukicha” na “si usiku si mchana” yanaonyesha kwamba mambo aliyoyatenda Nabii Isa hakuyafanya mara moja tu bali mara kadhaa japo yanasimuliwa mara moja tu. Kwa mawazo haya ni sawa kusema kwamba katika *Utenzi wa Nabii Isa* umedhihirisha matumizi ya usimulizi mosi, maana matukio mengi katika utenzi huu hayajarudiwa katika usimulizi.

2.3 Muda

Muda ni uhusiano wa kiwakati katika hadithi. Wamitila (2002: 143) anaeleza kuwa muda ni dhana inayorejelea uhusiano katika hadidhi, na swali la kujiuliza ni je, tukio limechukua kipindi kirefu au kifupi? Ili kujibu swali hili, kigezo kinachoweza kutumiwa ni kuangalia muda anaochukua mtu fulani kusoma hadithi fulani, jambo ambalo hapo awali tuliliangazia

kwamba ni gumu tukifahamu kwamba wasomaji tofauti huwa na kasi tofauti za kusoma. Kwa sababu ya tofauti hii, Rimmon-Kenan, (1983: 104), anapendekeza muda katika hadithi uangaliwe kupitia wakati-hadithi ambao hupimwa kwa dakika, saa, siku, wiki, miezi, au miaka, na wakati- matini ambao hupimwa kwa kurasa na mistari.

Uhusiano uliopo kati ya wakati-matini na wakati-hadithi unaweza kuathiri usimulizi wa hadithi, kwamba, kasi ya usimulizi wa matukio unaweza kuharakishwa au hata kupunguzwa katika matini. Hili hutokea pale ambapo tukio la muda mrefu linaelezwa kwa sentensi moja (kuharakisha kasi) au tukio la dakika chache kuelezwa kwa kurasa nzima (kupunguza kasi). Ili kuchanganua vyema dhana ya muda, Genette (1980: 95 -109), ameigawa katika sehenu nne; muhtasari, udondoshi, onyesho na mtuo.

2.3.1 Muhtasari

Katika muhtasari, kasi ya usimulizi huharakishwa. Rimmon-Kenan (1983: 104) anasema kuwa katika muhtasari kasi ya hadithi huharakishwa. Hili hutokana na kufupishwa kwa tukio fulani katika hadithi kwa maneno au kauli chache. Mfano mzuri wa hali hii katika *Utenzi wa Nabii Isa* ni Bi. Maryamu anazaliwa. (ubeti 37 - 40)

37. Nadhiri yake hakika,
Yote ikakubalika,
Naye akafurahika,
Mimba ilipotukia.

38. Kwa nia ya utakato,
Akashukuria pato,
Asiuone uzito,
Mimba na wake udhia.

39. Endapo yu furahani,
Kubwa isiyo kifani,
Hadi ilipoyakini,
Siku ya kujizalia.

40. Ingawa motto wake,
Alovyaa ni wa kike,
Pasi asibadilike,
Huzuni kumjilia.

Msimulizi anaelezea kutungwa mimba ya Bi. Maryamu hadi kuzaliwa kwake. Tangu kutungwa mimba hadi kuzaliwa kwa mwanadamu, kwa kawaida huchukua miezi tisa, na hatua za kuzaa hadi mtoto azaliwe huchukuwa saa kadhaa. Matukio haya yote ambayo yangechukua kipindi kirefu au muda mrefu yamefupishwa na kusimuliwa kwa maneno machache. (beti nne tu).

Mfano mwingine wa muhtasari tunauona katika malezi ya Nabii Isa, (ubeti 283).

Alilelewa na mammake,
Tokea uchanga wake,
Hadi ukubwani mwake,
Akawa mtu radhia.

Katika malezi ya mwanadamu toka kuzaliwa hadi ukubwani twafahamu kuwa mambo mengi hutokea. Kwanza, hatua za ukuaji wa mtoto, miezi mitatu ya kwanza mtoto hajitegemei, hubebwa au alale. Kisha aketi (mwezi wa nne na tano), atambae (kati ya mwezi wa sita hadi nane), kusimama (kati ya mwezi wa tisa hadi kumi na moja), kutembea (kati ya mwaka mmoja hadi mwaka na nusu), kuwa mtoto wa kujitegemea (kati ya miaka miwili hadi kumi), kijana barubaru (kati ya miaka kumi hadi kumi na saba) na hatimaye mtu mzima (miaka kumi na nane na kuendelea). Katika kulea si hatua hizi tu anazopitia mwanadamu kuna yale mzazi anapitia katika kumlea mwanawe, dhiki na furaha, magonjwa na mahitaji anayopaswa mzazi kumpa mwanawe. Ni mambo ambayo yanachukua miaka mingi. Mambo haya yote yameelezwa kwa ubeti mmoja.

2.3.2 Udondoshi

Udondoshi ni njia nyingine ya kudhihirisha muda. Katika udondoshi kasi huwa juu zaidi. Hapa tunapata kuwa wakati-hadithi unaendelea ilhali wakati matini ni nunge. Jambo hili linamaanisha kuwa kuna udondoshaji wa baadhi ya matukio au kutosimuliwa kwa matukio fulani katika matini. Hali inadhihirika katika njia mbili. Genette (1980: 106 - 108) anasema kuwa udondoshi unaweza kuwa bayana au usio kikimo. Yaani udondoshi bayana na udondoshi uso kikomo.

2.3.2.1 Udondoshi bayana

Katika udondoshi wazi (bayana) matini huonyesha wazi kiasi cha muda ambao umeachwa katika simulizi. Hapa msimulizi anataja kiasi cha muda ambao umepita kabla ya tukio jingine kutokea. kwa mfano miaka mitatu, miezi miwili, siku sita baadaye...na kadhalika. Aina hii ya udondoshi inadhihirika katika (ubeti 298)

Hivyo bin Maryamu,
Katika yake kaumu,
Thelathini akatimu,
Miaka alofikia.

Hapa msimulizi ameonyesha wazi kiasi cha muda ambao ulipita tangu kuzaliwa kwa Nabii Isa hadi kupewa au kuanza kazi yake ya utume. Kabla kufikia miaka hii, yapo mengi yalitokea katika maisha ya Nabii Isa mathalani kukua kwake, shida na taabu alizozipata katika kukua kwake. Mambo haya au matukio haya hayajaelezwa badala yake yamedondoshwa. Jambo hili la udondoshi bayana linaonyesha kuharakishwa kwa hadithi na uzito wa tukio au matukio. Vilevile udondoshi bayana umedhihirika katika ubeti wa 332.

ilitukia siku moja,
Isa akijikongoja,
Aona mtu mmoja,
Vya watu yuwaiba.

2.3.2.2 Udondoshi usio wazi au kikomo

Udondoshi huu kwa upande mwingine hupatikana pale ambapo muda haudhihiriki au haujitokezi wazi wazi, yaani kiasi cha mudawa mabadiliko ya matukio uliorukwa katika hadithi haujatajwa. Udondoshi huu hutumia maneno kama vile, miaka mingi ilipita, baada ya muda mrefu, daima, siku chache baadaye, milele, na kadhalika. Udondoshi usio wazi unadhihirika katika utenzi wa Nabii Isa katika (ubeti 328). Katika dondoo hii neno ‘daima’ limetumika kuonyesha muda ambao haudhihiriki au si mahususi. Aidha udondoshi usio wazi unadhihirika katika ubeti 539,

328. Safari zake akenda,
Daima yeye hupanda,
Kwenye maungo ya punda,
Vijijini kuzunguka.

539. **Katika siku zote,**
Atuonyazo sahibu,
Yapo mambo ya ghaibu,
Mngu humfunulia.

Dondoo hii (siku zote) haitupi muda kamili ambao Nabii Isa alikuwa akiwaonya wana wa Israeli. Inasemekana tu siku zote. Swali ni je siku zote za maisha yake au ni siku zote za utume wake? Jambo hili la wakati haliko wazi wala halionyeshi siku alizowaonya jamaa zake Wayahudi. Jambo hili la udondoshi linaonyesha kwamba yale matukio ambayo yamedondoshwa si ya muhimu katika hadithi lau yangekuwa basi yasingedondoshwa.

2.3.2.3 Udondoshi batini

Genette, (1980: 108), anasema udondoshi batini hudhihirika pale muda katika hadithi haujasemwa. Msomaji hugundua kwamba kuna udondoshi kwa kubaini mwenyewe kwamba kati ya matukio fulani kuna kiasi fulani cha muda umepita. Hili hubainika msomaji anapogundua kuwepo kwa mwanya baina ya matukio yanayofuatana kiwakati katika hadithi. Udondoshi batini huonyesha udondoshi usio wazi kwa sababu muda haujadhihirishwa au kutajwa kiasi chake. Kuna udondoshi batini kati ya kutoroka kwa yule mwizi aliyegunduliwa na Nabii Isa (ubeti 336) na pale mtunzi anaeleza juu ya maisha ya Nabii Isa (ubeti 337).

336. Yuli mtu akaona ,
Hoja zimezidiana.
Naye la kujibu hana,
Akawa atakimbia.

337. Sasa nawabainisha,
Ya bwana Isa maisha,
Hakuwa ‘jimakinisha,
Pamoja akatulia

Mtunzi haelezi baada ya mwizi kutoroka ni yapi yalitokea bali anaanza mara moja kueleza maisha ya Nabii Isa na kazi yake ya mahubiri. Hii inaonyesha wazi kwamba kuna undondoshaji ambao haujajitokeza kikamilifu. Hivyo hatutajua iwapo mwizi alitafutwa au la, kama alipatikana au la, na kama alipatikana nini kilimtendekeza, ama hata hakuna aliyeshughulika na jambo hilo.

2.3.2.4 Udondoshi dhahiri.

Udondoshi dhahiri unaweza wa wazi au usio wazi. Katika udondoshi huu muda katika hadidhi unaonyeshwa wazi, au mpito wa kiwakati kati ya matukio unabainika. Genette, (1980: 106). Mifano ya udondoshi huu ni kama tulivyoangazia katika udondoshi wazi hapo juu (ubeti 298).

Hivyo bi Maryamu'
Katika yake kaumu,
Thalathini akatimu,
Miaka alofikia.

Ambapo wakati unadhihirishwa kwamba umetimia miaka thelathini ndipo Nabii Isa akaanza kazi yake ya utume na udondoshi usio wazi, (ubeti 339) muda umedhihirika japo hauko wazi inasemekana tu wakati wote.

Si usiku si mchana,
Hana pa kutulizana,
Kila mji waonekana,
Enda akihubiri.

Kadhalika tunaweza kusema udondoshi kuonyesha kwamba matukio yaliyodondoshwa si ya muhimu katika hadidhi, hivyo ni yale tu ya muhimu ndiyo yanasimuliwa ili kuendeleza kukuza hadithi. Vinginevyo inatosha kuwa na simulizi zima linalochukuwa muda wa siku moja tu na inaweza kujaza matini ya takriban mamia na hata maelfu ya kurasa.

2.3.3 Onyesho

Kwa mujibu wa Wamitila, (2002: 143) onyesho ni njia ambayo huleta uigizaji katika matini yoyote ile. Njia mojawapo ya kuonyesha onyesho ni mazungumzo. Wahusika huonyeshwa mbele ya msomaji. Anaendelea kusema kuwa katika onyesho, wakati-hadithi na wakati-matini huwa sawa. Rimmon-Kenan, (2002: 54) anongezea kusema kuwa dayalojia ndiyo njia mwafaka ya kudhihirisha onyesho. Hii haimaanishi kwamba dayalojia ndiyo pekee ya kudhihirisha onyesho, hata mazungumzo ambayo hayana mfumo wa kidayalojia pia hudhihirisha onyesho.

Utenzi wa Nabii Isa umesheheni matumizi ya onyesho. Mazungumzo kati ya Bi. Maryamu na mjumbe wa Mungu yanaashiria matumizi ya onyesho.

123. Halafu akageuka,
Kwa kijana akatamka,
“kama unaaminika,
Ndiani niepukia
124. “Tena fanya taratibu,
Tusikosane adabu,
Siutaki uswahibu,
Fasiki na mazoea.
- 125.”Na wala usijaribu,
Kufika pangu karibu,
Bora name jitanibu,
Wende unayeendea.
126. “kama waicha ghadhabu,
Ya Molao kukusibu,
Hiyo siku ya hisabu,
Siwe kunikurubia.
127. “Nikwambiayo fahamu,
Mimi bibi Maryamu,
Sina kijicho na hamu,
Kuitazama dunia.”
128. “Ndipo naye mvulana,
Kwa hishima akanena,
“Bibi nisamehe sana,
Kwako sina mbaya nia.”
129. “Natubu kwako kiumbe,
Sikuja nikukurumbe,
Nimekuja na ujumbe,
Utokao kwa Jalia.
130. “Haya ninayotamka,
Nakwambia ya hakika,
Ujue ni malaika,
Mngu namtumika.
- 131.”Sikia nakweleza,
Sikufika kukutweza,
Nimekuja tekeleza,
Amri yake Jalia.

Mwandishi ametumia pia onyesho ambalo si dayalojia japo ni mazungumzo. Kwa mfano mazungumzo ya mtume Zakaria alipotoa suluhisho la ni nani anastahili kumlea Binti Imrani. Katika onyesho hili kuna mchanganyiko wa mazungumzo japo yote yanadhihirisha onyesho moja. (ubeti 56 – 66) ni masimulizi ya msimulizi akionyesha vile hali ilivyokuwa Maryamu akitafutiwa mlezi. Katika (ubeti 67 - 72), ni mazungumzo ya zakaria akiwa mbele ya umati akieleza jinsi yeye anafaa kumlea Bi. Maryamu na kutoa ushauri wa namna mlezi atakavyopatikana bila kulaumiana. Kasha yanafuata masimulizi ya namna shauri lilivyopokelewa na kutekelezwa. (ubeti 73 - 74). Zakaria anaendelea na mazungumzo yake (ubeti 75 - 84) hadi kura inapomwangukia kumlea Maryamu binti Imrani.

Onyesho huwa na matukio yenye mnato au mvuto kwa msomaji. Aidha dayalojia yake huwa na matini ndefu kama tunavyoona katika mfano tuliotoa hapo juu, japo sikila wakati. Kadhalika onyesho linaweza kuashiria dhamira na maudhui ya kazi ya fasihi. Kwa mfano, onyesho tulilotoa hapo juu la mazungumzo baina ya Bi. Maryamu na mjumbe wa Mungu yanaibua maudhui ya maadili. Aidha sifa za wahusika zinabainika. Mathalani Bi. Maryamu katika dayalojia hii anasawiriwa kama msichana anayejiheshimu, mcha Mungu, mwenye tabia njema n.k. naye mjumbe wa Mungu kama mtaratibu, mwenye subira na mvumilivu.

2.3.4 Mtuo

Kama vile udondoshi ni udhihirisho wa kasi ya juu, mtuo ni udhihirisho wa kasi ya chini katika hadithi. Mtuo katika simulizi hutokea wakati msimulizi anaacha kueleza hadithi na kuingiza maelezo tofauti na yale yanayoendeleza mtiririko wa hadithi. Maelezo haya yanaweza kuwa nje ya hadithi au hata hayahitajiki katika simulizi husika. Mwazo haya ni sawia na ya Wamitila, (2003: 147)

Mtuo hueleza jinsi ya kudhihirika kwa wakati au kasi- hadithi. Kinaratolojia tunasema kuwa mahali Fulani pana mtuo ikiwa wakati-matini hauelekei kupatana na wakati hadithi. Mtuo hupatikana kutokana na maelezo au mawazo ya pembeni ya msimulizi.

Genette, (1980: 99), anasema kuwa mtuo hutokea pale ambapo msimulizi huacha kwa muda mtiririko wa hadithi na kutoa maelezo ambayo wakati mwingine hayana uhusiano na hadithi au hata hayahitajiki.

Namna nyingine ya kudhihirisha mtuo ni maelezo ya wasifu wa mhusika. Katika namna hii ya kudhihirisha mtuo, msimulizi anaweza kueleza sifa za mhusika fulani kitabia au kimaumbile. Mtunzi wa utenzi wa Nabii Isa ameeleza sifa za Nabii Isa. (ubeti 691 - 698).

691. Nabii mzungupule,
Isa pindi umuole,
Alikuwa ni mpole,
Kati yao insia.

692. Ungeweza kumjua,
Bwana huyu wa uluwa,
Kimo chake kilikuwa,
Wastani Masihia.

693. Si mfupi si mrefu,
Si mwembamba si waswifu,
Si mnene kuarifu,
Umbo ukimwangalia.

694. Na rangi yake rasuli,
Ya chake kiwiliwili,
Wekundu hana kamili,
Weupe mchanganyia.

695. Hakuwa mwenye kiburi,
Hakuwa na ujeuri,
Kwa hali ya tahayuri,
Chini akiangalia.

696. Alama ya uchaMngu,
Muumba nchi na mbingu,
Ni nadra mlimwengu,
Juu kujitizamia.

697. Na upole wake huu,
Hakuyapenda makuu,
Kukalia juujuu,
Isa hakupendelea.

698. Juu ya yake mapenzi,
Apendayo Mwenyezi,
Hutiririkwa machozi,
Ya kicho kumzidia.

Baada ya kueleza jinsi Nabii Isa alivyofanya kazi yake, mtunzi anamalizia kwa kuonyesha dhiki aliyopata Nabii Isa na wafuasi wake. (ubeti 690), kisha mtuo unatokea. (ubeti 691 - 698). Hapa mtunzi anaelezea sifa za Nabii Isa. Hadithi inaanza tena mtunzi anapoeleza shughuli ambazo Nabii Isa na wafuasi wake walifanya katika kazi yao ya kuhubiri.

Kadhalika baada ya mjumbe wa Mungu kuzungumza na Bi. Maryamu, ambayo yanamalizikia katika (ubeti 155), mtunzi anaweka mtuo kwa kueleza zaidi kwa nini Bi. Maryamu hakuridhia ujumbe ulioletwa na mjumbe wa Mungu kwa urahisi. (ubeti 156 - 164) kisha anarudia hadithi Maryamu anapomjibu mjumbe wa Mungu (ubeti 165) na hadithi inaendelea.

2.4 Mpangilio

Katika hadithi matukio hupangwa na kufuatana kiwakati. Genette,(1980: 34) anaeleza kuwa mpangilio ni uhusiano baina ya mfuatano wa matukio katika hadithi. Dhana hii ya mpangilio inaonyesha jinsi matukio yanavyohusiana katika kutendeka kwao moja baada ya jingine katika hadithi. Yaani matukio yanaweza kusimuliwa katika hadithi kulingana na vile yanavyotokea kiwakati. Hata hivyo matukio katika hadithi yanaweza kusimuliwa kwa namna ambayo inakiuka mfuatano wao kiwakati. Hivi nikusema kwamba tukio ambalo limetokea kwanza likasimuliwa mwisho katika hadithi au la mwisho kusimuliwa kabla ya lile la kwanza. Hali hizi huzua hali za urejeshi na uelekezi mtawalia. Hali hii ya matukio kusimuliwa kwa mpangilio wa kiwakati hujulikana kama anakroni. Utafiti huu utachunguza aina mbili za anakroni, ambazo ni pamoja na analepsia (mbinu rejeshi) na prolepsia (mbinu elekezi).

2.4.1 Analepsia

Analepsia ambayo pia inaitwa mbinu rejeshi, ni mbinu ambapo masimulizi ya matukio yaliyotokea nyuma yanasimuliwa kabla ya yale yaliyoyatangulia kutendeka. Wamitila, (2003: 117) anaeleza kuwa mbinu rejeshi hutumiwa na waandishi kueleza matukio yaliyotokea nyuma ya wakati wa hadithi. Naye Rimmon-Kenan, (2002: 46) anasema kuwa analepsia ni usimulizi wa tukio katika hadithi ambapo tukio la mbele linasimuliwa kabla ya yale yaliyotendeka kabla yake. Analepsia hutegemea anayesimulia kuhusu analepsia na

sehemu ya usimulizi ambayo analepsia inarejelewa. Kwa kufuata misingi hii tunapata aina tofauti tofauti za analepsia. Kama alivyoeleza Genette (1980: 48) kama ifuatavyo; analepsia ya nje (external analepsis), analepsia ya ndani (internal analepsis), analepsia met (mixed analepsis), analepsia tawasifu (homodiegetic analepsis) na analepsia wasifu (heterodiegetic analepsis).

2.4.1.1 Analepsia ya nje.

Mbinu hii ya usimulizi ambayo huhusisha matukio ambayo kiwakati yako nje ya wakati wa mwanzo wa hadithi. Wamitila, (2003: 117). Aidha analepsia ya nje kama asemavyo Genette, (1980: 49) masimulizi ya matukio ya mwanzo kabla ya hadithi yenyewe kuanza

Utenzi wa Nabii Isa unianza kwa kusimulia kuzaliwa kwa mama yake Bibi Maryamu binti Imrani (ubeti 9 - 55). Sehemu hii inaonyesha analepsia ya nje. Analepsia hii inatujulisha asili ya Nabii Isa ambaye utenzi huu unasimulia kumhusu. Usimulizi huu umeturudisha nyuma ili kujua ukoo au asili yake Nabii Isa, hivyo kufanya kisa hiki kueleweka vyema. Maelezo haya aidha yanatusaidia kumfahamu vyema Nabii Isa ambaye tunasoma kisa chake. Kwa maelezo haya tunapata kuwafahamu babu na bibi yake Nabii Isa. Kadhalika analepsia nyingine ya nje katika utenzi huu ni masimulizi ya kuzaliwa Bibi Maryamu binti Imrani ambaye ndiye mama yake Nabii Isa ambaye utenzi huu unaelezea kisa chake. (ubeti 56 - 109). Hadithi yenyewe inianza jinsi Nabii Isa alivyotokea. (ubeti 4) kama aelezavyo msimulizi katika dibaji.

Nisimulie kwa hamu.
Itangae hii ilimu,
Kisa cha binadamu,
Isa alivyotukia.

2.4.1.2. Analepsia ya ndani

Analepsia ya ndani ni masimulizi ya matukio yanayotokea baada ya kuanza hadithi lakini hayasimuliwi wakati yalipotendeka. Husimuliwa baadaye katika hadithi. Kama asemavyo Wamitila (2003, 117), kwamba ni mbinu rejeshi ambayo huhusisha matukio yaliyopita lakini yasiyokuwa ya kabla ya wakati ianzapo hadithi. Mtunzi wa utenzi wa Nabii Isa haijatumia mbinu hii.

2.4.1.3. Analepsia mseto

Analepsia mseto kwa ufupi ni mchanganyiko wa analepsia ya ndani na analepsia ya nje. Yaani ni analepsia ambayo inasimulia matukio yaliyotendeka kabla ya mwanzo wa hadithi na kuendelea hadi mwanzo wa hadithi na kisha kuvuka mwanzo wa hadithi hiyo. Genette (1980: 49) anaeleza

Analepsia mseto ni masimuli ya matukio ya kabla
ya mwanzo wa hadithi na ambayo huendelea hadi
kuvuka mwanzo wa simulizi.

Katika *Utenzi wa Nabii Isa* kuna analepsia mseto pale ambapo jamaa za Bibi Maryamu wanamwelezea Maryamu sifa za wazazi wake. Analepsia hii inaturudisha nyuma hadi maisha ya wazazi wa Bi. Maryamu ambao kwa sasa hawapo duniani washaaga. Ni wakati ambao Bi. Maryamu alikuwa mdogo chini ya malezi ya wazazi wake. (ubeti 247, 249, 250).

247. “Ewe Bibi Maryamu,
Wazazi wako fahamu,
Hawakuwa wakidumu,
Uchafu kukurubia.

249. Jambo hili la ushenzi,
Wazazi wako vipenzi,
Hawakuwa wapotezi,
Sifa kujibanangia.

250. “ kila sifa ya ulezi,
Walikupa kwa mapenzi,
Ulikuaje mzazi,
Nawe hujafunga ndoa?

Mfano huu tuliotoa wa analepsia mseto inatoa sifa za wazazi wa Bibi Maryamu, hivyo kutufanya kuelewa chanzo cha maadili ya Bibi Maryamu.

2.4.1.4. Analepsia wasifu

Analepsia wasifu hutoa taarifa kuhusu matukio yaliyopita juu ya mhusika mwingine ambaye hayupo katika masimulizi hayo wakati yanaendelea, tukio jingine au hadithi nyingine ambayo haihusiani na mkondo wa hadithi inayosimuliwa kwa wakati huo. Aina hii ya analepsia inajitokeza katika *Utenzi wa Nabii Isa*, katika mazungumzo ya walimu wa kiyahudi

wakisema uongo au kumfitini Nabii Isa kwa wakuu wa Roma. (ubeti766, 767,768, 770 - 774).

766. “Enyi wakuu wa Roma,
Yashuka yenu hishima,
Kwa kuwa tukitizama,
Isa yuwawazidia.

767. “kila kukipambazuka,
Majambo yabadilika,
Na watu wetu hakika,
Ni wenye kutukimbia.

768. “Isa yuwawarubuni,
Kuwabadili imani,
Wawaasi makuhani,
Makanisa yao pia.

770. “Isa ni mtu sabasi,
Kadhalika ameasi,
Watawala awagusi,
Serekali na raia.

771. “Kanuni za makanisa,
Hazifuati kabisa,
Asema zina makosa,
Zapoteza watu njia.

772. “Tena kwa watu husema,
Sisi kutupa lawama,
Kutwambia si lazima,
Makanisa kuyajua.

773. “Sababu hayo aseme,
Ni kutaka asimame,
Awe yeye mfalume,
Na sisi kuwa raia.

Kupitia mazungumzo haya tunapata maudhui ya uongo, usaliti na kupenda cheo au mamlaka. Aidha tunapata taswira ya hatari ambayo inayomkabili Nabii Isa.

2.4.2. Prolepsia

Pia wataalamu wengine huiita mbinu elekezi. Prolepsia ni mbinu ya usimulizi ambapo msimulizi husimulia matukio yatakayotokea baadaye lakini anayasimulia sasa katika hadithi.

Yaani ni mbinu inayohusisha kuleta mapema matukio yatakayotendeka baadaye katika hadithi. Kadhalika ni mbinu ambayo huleta matukio ya baadaye katika hadithi kabla ya matukio ya sasa kusimuliwa. Hali ambayo huleta ukiushi kutoka kwa hadithi yenyewe. Kauli hii inakubaliana na ya Wamitila, (2003: 117) kuwa; “ni dhana inayotumiwa kuelekeza hali ambapo mwandishi anatupa picha ya matukio ya mbele katika hadithi. Aghalabu kwa kutuonyesha mwisho wa hadithi inayohusika. Ni njia mojawapo inayomtia msomaji taharuki ya kutaka kujua sababu ya hali inayoonyeshwa. Aidha ni njia ya kuhakikisha kuwa hamu ya msomaji haijifungi kwenye kujua mwisho wa hadithi bali anayozingatia na kuyawaza mambo yaliyopo anapoisoma kazi fulani.”Kama ilivyo kwa analepsia imeainishwa kama prolepsia kama, prolepsia ya ndani, prolepsia ya nje, prolepsia mseto, prolepsia tawasifu na prolepsia wasifu.

2.4.2.1 Prolepsia ya ndani

Prolepsia ya ndani ni mbinu ya kusimulia (ma)tukio ambayo yatatendeka baadaye katika hadithi kabla hadithi yenyewe kufika mwisho. Ni kwamba matukio yanayosimuliwa ni mojawapo ya matukio katika hadithi. Mojawapo ya matukio yanayodhihirisha prolepsia ya ndani katika utenzi wa Nabii Isa, ni wakati Bibi Maryamu anakutana na mjumbe wa Mungu. Katika mazungumzo yao mjumbe wa Mungu anamueleza Bibi Maryamu kwamba atapata mimba na kumzaa kijana. Jambo ambalo Bibi Maryamu analitilia shaka akifahamu fika kwamba haliwezekani kwa sababu yeye bado ni msichana mdogo na hajafunga ndoa wala kuonana na mwanamume kimwili. (ubeti 132, 147 na 148)

132. “Menituma Subuhana,
Mimi nawe kuonana,
Ili nikupe kijana,
Mtukufu kukujia.

147. “Naye atakuwezesha,
Kijana kukuzalisha,
Bila kukujumuisha ,
Na mume kukungilia.

148. “Mungu amekutakasa,
Hu mchafu huna kosa,
Nawe kumzaa Isa,
Ndivyo amekujalia.

Genette (1980: 68) anasema kwamba prolepsia haina umaarufu katika kazi nyingi za kifasihi, utenzi wa Nabii Isa unadhihirisha hili. Mtunzi wa *Utenzi wa Nabii Isa* ametumia aina moja pekee ya prolepsia na kuacha zile nyingine.

2.5. Hitimisho

Katika sura hii tumejadili kipengee cha wakati pamoja na aina zake mbali mbali. Tumeona kwamba kipengee hiki ni muhimu sana katika kazi ya fasihi hususan simulizi, kwa sababu matukio yote hutokea kiwakati. Katika kujadili kipengee hiki cha wakati tumegundua kuwa si vipengee vyote vinavyohusiana na wakati vimetumika. Mtunzi yuko nauhuru wa kutumia vingine na kuacha vingine.

Katika *Utenzi wa Nabii Isa* kipengee cha wakati kimetumika japo kwa kiasi. Katika kipengee cha mpangilio, mbinu ya analepsia imetumika kikamilifu isipokuwa analepsia tawasifu, ilhali katika kipengee cha prolepsia mtunzi ametumia mbinu ya prolepsia ya ndani pekee.

Kadhalika vipengee vya muda, muhtasari, mtuo umara na onyesho vimedhihirika katika utenzi huu wa Nabii Isa. Vipengee hivi vimetusaidia kuuelewa vema utenzi huu.

SURA YA TATU

UWASILISHAJI USEMI

3.1 Utangulizi

Katika kazi yoyote ya fasihi lugha ni kipengee muhimu. Lugha ndiyo itumiwayona waandishi ili kuwasilisha ujumbe wao au fikira zao. Katika kazi yoyote ya fasihi lugha huhusishwa na wahusika. Hii ni kwa sababu mtunzi hutumia wahusika kuwasilisha ujumbe wao na ndio watumizi wa lugha katika kazi hiyo. Katika kuwasilisha ujumbe, njia mbili hutumika, usemi halisi na usemi wa taarifa, nakuhusiana na kauli hii tunakubaliana na maoni ya Wamitila, (2008: 96) kwamba, “Jinsi lughainavyowasilishwa katika kazi ya fasihi ni swala muhimu sana katika kazi ya uchanganuzi wa fasihi. Usemi unaopatikana katika kazi ya fasihi unaweza kuwasilishwa kwa njia kadhaa. Njia kuu ni maelezo (ambayo matukio yanaelezwa au kusimiliwa jinsi yalivyotokea) ya msimulizi. Hii ndiyo ambayo inaelezwa na wananadharia wa naratolojia kama daigesia. Kinyume chake ni pale ambapo lugha ya wahusika inawasilishwa kwa njia iliyo wazi. Wahusika wanajibizana, na kwa njia hii kuakisi hali halisi kama ilivyo katika drama. Hali hii hujulikana kama muhakati au mimesia”.

Kama ilivyo katika riwaya, wahusika katika utenzi huzungumza na wanapozungumza usemi halisi hutumika. Hii hudhihirishwa kwa kutumia nafsi ya kwanza katika maongezi yao kwa kutumia viwakilishi nafsi vyake mathalanni (umoja) au **tu** (wingi). Kadhalika kwa kutumia viwakilishi vya nafsi ya tatu ambavyo ni **a** (umoja) au **wa** (wingi).

Kimsingi, katika usemi halisi tunanukuu maneno ya msemaji moja kwa moja ilhali katika usemi wa taarifa tunatumia maneno yetu wenyewe kueleza kilichosemwa na mtu mwingine. Usemaji huu wa kutumia usemi halisi na ule wa taarifa tumeujadili katika sura hii kama mojawapo wa vipengee vinavyoangaziwa katika mada yetu ya utafiti.

3.2 Usemi halisi na mawazo halisi

Wamitila, (2008: 97) anaeleza kuwa usemi halisi ni uwasilishaji wa maneno yaliyotamkwa na msemaji kama alivyoyatamka kwa matumizi ya alama za mtajo. Katika usemi halisi, kuwasilisha maneno au fikira aidha kitenzi kiarifu lazima kitumike. Mathalani “akasema”, “akawaza”, na kadhalika. Jambo hili tunalionga katika *Utenzi wa Nabii Isabaada* ya kifo cha mama yake bi. Maryamu, baba yake alitafuta mtu ambaye angemlea Maryamu. Watu wengi

walikuja kuomba wakubaliwe kumlea Maryamu. Katika kujadili jambo hili Zakaria alitoka kuongea na umati kwamba yeye ndiye anayefaa kumlea Maryamu. (Ubeti 66, mshororo 4) “ watu **akawaambia**”Neno‘akawaambia’ ni kitenzi kiarifu kilichotamkwa na msimulizi ambacho kinafuatwa na maneno halisi ya Mtume Zakaria (ubeti 67 - 72) ambayo yameakifishwa na alama za mtajo.

67. “watu tusikilizaneni,
Fujo natuliacheni,
Kijana huyu soteni,
Kumlea ni sawia.

68. “kwa ajili sote sisi,
Kwa Mola wetu mkwasi,
Ni ndugu moja halisi,
Kwa dini hata sharia.

69. “lakini upande wangu,
Maryamu ni mwanangu,
Maleziye mlimwengu,
Mimi nasitahilia.

70. “tuyaacheni maneno,
Tuazimu mapatano,
Juu ya ulezi huno,
Shauri nitawaambia.

Mfano mwingine tunaupata pale Maryamu alipomjibu Mtume Zakaria baada ya kumuuliza kuhusu vyakula anavyokula vilitoka wapi. Mtunzi anayanukuu maneno yaliyotamkwa na Bi. Maryamu jinsi alivyoyatamka bila kuyabadilisha. Kitenzi kiarifu kinaanza katika ubeti wa 95, mshororo wa 1. “Maryamu **akasema**,”Halafu maneno ya au jibu la Maryamu linafuata. (ubeti 96)

“Hakika hii neema,
Yatokana na Karima,
Mwenye kuruzuku umma,
Pasi na kuwakisia.”

Katika sehemu ya tatu, mazungumzo kati ya mjumbe wa Mungu na Bi. Maryamu pia yanadhihirisha usemi halisi. (ubeti 123 - 127) Bi. Maryamu anamzungumzia Mtume wa Mungu. (ubeti 128 - 132) Mtume wa Mungu anamzunguzia Bi. Maryamu. Mazungumzo

haya yanaendelea hadi ubeti 176. Hii ni baadhi ya mifano ya usemi halisi katika utenzi wa Nabii Isa ipo mifano mingine mingi ambayo hatutaweza kuiandika yote.

Mawazo halisi nayo hutokea pale ambapo mtunzi ananukuu mawazo au fikira za mhusika. Hapa hakuna kilichotamkwa kwa mdomo bali kile kilicho ndani ya akili ya mhusika. Dhana ambayo Wamitila anaiita mtindo au mawazo halisi. Kwa mfano, baada ya Mtume Zakaria kujibiwa na Bi. Maryamu kuhusu muujiza wa kuletewa vyakula alitamka moyoni. (ubeti 98).

Akatamka moyoni,
“yatokana na Karima,
Mwana huyu ni yakini,
Metukuzwa ni Jalia.”

Hii inadhihirisha kwamba Mtume Zakaria hakutamka kwa mdomo bali haya ni mawazo yaliyokuwa ndani ya akili yake. Kadhalika dua ya Bi. Maryamu alipokutana na Mtume wa Mungu akiwa na hofu moyoni asijue kusudi lake kwa maana hakujua kijana anayemuona alikuwa ni nani, aidha ni dhihirisho ya mawazo halisi. (ubeti 119 - 122).

119. Akaomba “ya Rabbana,
Muumba mtajikana,
Nikinga na wenye lana,
Wasiwe kunandamia.

120. Mimi hapa msichana,
Nawahofu wavulana.
Kwani tukifuatana,
Watu wataniulizia.

121. Watayazua machafu,
Kunidhani ni dhaifu,
Mwanamke mzinifu,
Mwenye utovu wa haya.

122. Nakuomba Subuhana,
Hususa kwa huyu bwana,
Ambaye unamuona,
Awe na njema tabia.”

Kwa muhtasari tunaweza kusema kwamba maneno au mawazo halisi yanapowasilishwa hufungwa kwa alama za mtajo na hutangiliwa na kufuatwa na ni nani anayesema au

kutamka maneno hayo. Maelezo ya ni nani anayesema yanadhihirisha kuwepo kwa msimulizi. (Kishazi kiarifu).

Katika usemi halisi au mawazo halisi maneno ya msimulizi hutoa au kuonyesha mtazamo au hisia za msimulizi ambazo kwa kiasi kikubwa huathiri msomaji. Ubeti wa 119 umeanza kwa neno ‘akaomba’ neno hili linamjulisha msomaji kwamba dua inafuata, hivyo tabia yake ya usomaji itabadilika na kuchukuwa hali ya utulivu na heshima kwa Mungu akionekana kana kwamba ndiye anayetoa dua hiyo. Katika ubeti wa 142, “ Maryamu mshindani akaamba,” kishazi hiki kinamtambulisha Mariamu kama mtu mshindani asiyesemezekana badala ya ile taswira ya kwanza ya mtu aliyejaa neema na heshima na tabia ya kupendeza. Ubeti wa 203, “mwana akamliwaza” kiarifu hiki kinampa msomaji hisia za kumhurumia Bi. Maryamu na kumsawiri kama mtu dhaifu na mhitaji.

3.3 Usemi halisi huru na mawazo halisi huru

Tumetangulia kusema kwamba katika usemi halisi maneno ya msemaji hunukuliwa na pia kishazi kiarifu hutumika. Hutokea hali ambapo sifa hizi mbili katika usemi au moja inaondolewa. Jambo hili linapotokea katika uwasilishaji halisi, basi matokeo yake huwa ni usemi halisi huru. Wamitila, (2008: 99) anadhihirisha haya kwa kusema kuwa,

usemi halisi huru hutokea pale ambapo vishikizi vya kauli ya msemaji (maneno yanayofuata dondoo au nukuu) na alama za nukuu za kuonyesha kuwa huo ni usemi halisi zimeondolewa.

Usemi huu unadhihirika katika ubeti wa 372 – 376.

372. “Mimi ninao ujuzi,
Wa kujua uandazi,
Mulavyo kwenye makazi,
Na muyafanyayo pia.

373. “tamtaja alenacho,
Asubuhi amezacho,
Na jioni akilacho,
Vyote kumuhisabia.

374.” kadhalika na akiba,
Wingi wake na uhaba,
Mahali munapoziba,
Maficho tawatajia.

375. “na vitu mulivyonavyo,
Vya maana na vya ovyo,
Kupokea na mupavyo,
Vyote tawaaridhia.

376. “na atakaye hakika,
Kama ninavyotamka,
Namuomba kuinuka,
Vyake kumuhisabia.”

Mifano mingine zaidi ni katika ubeti wa 347 – 351, 366 na 387 – 391. Katika mifano hii alama za mtajo zipo lakini kishazi kiarifu hakipo, hivyo kuunda usemi halisi huru. Usemi halisi huru huleta athari ya kuharakisha mazungumzo. Mhusika katika usemi halisi huru huongea na hadhira moja kwa moja bila msimulizi kuingilia kati. Aidha msomaji anaweza asielewe maneno haya yametamkwa na nani au hata kutoa uamuzi usio sahihi kuhusu mhusika aliyetamka maneno haya. Barry, (1993: 237) anasema, “usemi halisi huru unaweza kuleta utata wa kuelewa ni nani msemaji iwapo kishazi kiarifu hakipo.”

Mbali na usemi halisi huru ambao ni matamshi halisi ya msemaji ambayo yameondolewa ama vinukuu au kishazi kiarifu, mwandishi anaweza kuwasilisha kilicho katika akili ya mhusika au mawazo au fikira zake. Mwandishi anapowasilisha fikira au mawazo ya mhusika kwa kutumia usemi halisi ulio huru basi husemekana kutumia mbinu ya mawazo halisi huru. Sawia na usemi halisi huru, mawazo halisi huru kishazi tangulizi au kiarifu na alama za mtajo huondolewa au mojawapo ya sifa hizi kuondolewa. Kauli hii inathibitishwa na Wamitila, (2008: 101), anasema,

mtindo ama mawazo halisi huru hutokea pale ambapo
mawazo au fikira za mhusika zinawasilishwa kwa
mtindo halisi au usemi halisi bila ya kuwepo kwa alama
za mtajo au vishazi vinavyofuatia kauli halisi.

Wamitila anaendelea kueleza kuwa mawazo au fikira za mhusika huwasilishwa katika wakati uliopo na kwa nafsi ya kwanza. Kutokuwepo kwa kishazi tangulizi kuna hakikisha kwamba

matini inatiririka bila ya kukatizwa na msimulizi anayeelekea kudhibiti matukio. Kwa mfano katika *Utenzi wa Nabii Isa* Bi. Maryamu anapokuwa akirudi kwao, hofu inamkabili ya jinsi atakavyopokelewa na jamaa zake na jinsi atakavyowaeleza ili waelewe na kusadiki kuhusu mwana aliyempata. Mambo haya yote yanampitikia katika akili yake. Mzenga anayawasilisha mawazo ya Bi. Maryamu kwa kutumia mbinu hii ya mawazo halisi huru. (ubeti 222 - 225).

222. “kiapo chochote kile,
Ningaapa kwa milele,
Katu hawatasadiki,
Mawi watanizushia.

223. “Kila ambalo ni chafu,
Lawama na takishifu,
Ndiyo wajayo arifu,
Wengine kuhadithia.

224. “Hino ndiyo yangu hofu,
Moyo una takilifu,
Kwa wangu utakatifu,
Watu kunisimangia.

225.”Ewe Isa mwanangu,
Mwana mpewa ni Mungu,
Wanambiaje mwanangu,
Huzuni imeningia?”

3.4 Usemi wa taarifa na mawazo taarifa

Kadhalika mtunzi anaweza kutumia usemi wa taarifa katika kuwasilisha ujumbe wake au kusimulia hadithi yake. Anapotumia usemi huu, viwakilishi vya nafsi ya tatu hutumika. Usemi wa taarifa huendana na usimulizi wa nafsi ya tatu ambao huangazia hadithi kwa mtazamo wa nje. Katika mtazamo huu, kuna wakala wa usimulizi ambaye yuko nje ya hadithi. Yeye husimulia matukio katika hadithi na wala si mhusika. Aidha katika usemi wa taarifa hatunukuu maneno ya msemaji moja kwa moja bali tunatumia maneno yetu kueleza kilichotamkwa na mnenaji. Hapa alama za mtajo au vishazi viarifu havitumiki. Kama asemavyo Wamitila, (2008: 102 – 3)

usemi wa taarifa hauna matumizi ya alama za nukuu na huwepo maneno yanayoonyesha kuwepo kwa usemi wa taarifa. Aidha huwa na maneno kama vile “kwamba.” Matumizi ya viwakilishi vya nafsi ya kwanza na ya pili – “mimi” na “wewe” huchukuliwa na viwakilishi vya nafsi ya tatu, “yeye.” Pia viwakilishi vya mahali na wakati hubadilika na pia pana mabadiliko kuhusiana na mwelekeo wa vitenzi kutoka “kuelekea” hadi “mbali na.

Mtunzi amedhihirisha usemi huu katika *Utenzi wa Nabii Isa* ambao umesheheni kuwepo kwa usimulizi wa nafsi ya tatu toka mwazo hadi mwisho. k. m (ubeti 20 - 41). Haya ni maelezo ya matukio ya asili ya Nabii Isa, jinsi mama yake Bi. Maryamu alivyozaliwa.

20. Nakwake yeye nyumbani,
Yuli na mke mwendani,
Ibada hawezekani,
Mcha Mungu maridhia.

21. Imrani alikuwa,
Kiongozi wa kuchiwa,
Hivyo Imrani akawa,
Aqsa kiswalishia.

22. Ni mkewe msifika,
Wakipendana hakika,
Imani kawaridhika,
Ibada kusimamia.

23. Mke yalipomzidi,
Mahabakwake wadudi
Imani akashitadi,
Mume kumfuatia.

24. Wenende msikitini,
Aqsa wajimakini,
Wamuabudu Manani,
Na kumtii sawia.

25. Bali kuwa ni nisai,
Jambo alilotumai,
Akawa yeye hafai,
Msikitini kungia.

Katika usemi wa taarifa baadhi ya maneno hubadilika. Kwa mfano, wakati wa kitenzi, vionyeshi, vielezi vya mahali, vimilikishi miongoni mwa mengine. Mfano tuliotoa unaashiria jambo hili. Kwa mfano, viwakilishi nafsi vilivyotumika ni vya nafsi ya tatu, mathalani, “a”, “wa” na “yeye.” Aidha vimilikishi pia ni vya nafsi ya tatu, kwa mfano, “yake” na “wake.” Na kadhalika. Mifano mingine inayodhihirisha usemi wa taarifa ni pale ambapo msimulizi anaelezea Imrani alivyotafuta mtu wa kumlea bintiye Bi. Maryamu baada ya kufiwa na mkewe. (ubeti 56 – 60, 62 – 66, 84 -91). Pia maelezo ya matukio ya aliyaona Zakaria wakati akimlea Bi. Maryamu anaashiria usemi huu. (ubeti 100 - 103).

Mifano ya usemi wa taarifa katika *Utenzi wa Nabii Isa* ni mingi na hatuwezikitaja yote kwa sababu yote ina ashiria jambo moja na ina matumizi sawia aliyotumia mwandishi. Kadhalika mwandishi anaweza kuwasilisha mawazo ya mhusika katika usemi wa taarifa. Mwandishi anapofanya hivyo huzua dhana nyingine ya mawazo au mtindo taarifa. (ubeti 92).

Zakaria akiwaza,
Mambo yamemduwaza,
Akaona hapo Mweza,
Mahali hapa kungia.

Mwandishi pia anaeleza hofu aliyokuwa nayo Bi. Maryamu alipomuona kijana (Mjumbe wa Mungu) na jambo alilolifanya. (ubeti 117)

Akawa na takilifu,
Moyoni na nyingi hofu,
Kwa huno ukusudi,
Wa mtu kumjia.

Hisia za mjumbe wa Mungu ni mfano mwingine wa mtindo taarifa, ambazo mwandishi anazielezea. (ubeti 139)

Malaika akahisi,
Bibi huyu ni halisi,
Ni katika watakasi,
Metakaswa ni Jalia

3.5 Usemi wa taarifa huru na mawazo taarifa huru

Hii ni aina nyingine za uwasilishaji usemi katika hadithi. Usemi taarifa huru (U. T. H), unatoa ripoti ya maneno au kueleza maneno kama yalivyotamkwa na msemaji ilhali mawazo taarifa huru (M. T. H) ni maelezo ya mawazo ya mhusika. usemi wa taarifa unapoafanyiwa mabadiliko kwa kuondoa maneno ya yanayoonyesha usemi wa taarifa, na kudumisha baadhi ya sifa zinazohusishwa na usemi halisi, zao lake huwa usemi taarifa huru. Hapa msimulizi wa nafsi ya tatu anatumia wakati uliopo kusimulia hadithi. Usemi huu unadhirika katika *Utenziwa Nabii Isa* pale msimulizi anaposimulia au kueleza jinsi Nabii Isa alivyopewa kipawa cha utume. (ubeti 300 - 313).

300. Akaambiwa: ya Isa,
Baada Mtume Musa,
Wewe pia ni hulasa,
Utume kushikilia.

301. Uongozi madhubuti,
Wa kuongoza umati,
Shikilia taurati,
Ya Musa kuirudia.

302. Maongozi yayohayo,
Wewe endelea nayo,
Iwe ni makusudiyo,
Watu wako kufunzia.

303. Wana wa Israili,
Mambo wameyabadili,
Sharia hawajali,
Hawataki kitumia.

304. Mambo nilowakataza,
Ndiyo wanayofanyizia,
Kasha wamependekeza,
Maovu kufuatia.

305. Sababu ya waalimu,
Wakubwa na maimamu,
Wamepindua hukumu,
Wanyonge wawaonea.

306. Yawapasayo kulipa,
Ushuru wanaukwepa,
Wanyonge wapelekwa kappa,
Wabora wawalipia.
307. Kwa nguvu wawaamuru,
Kuwalipisha ushuru,
Watu wanawahusuru,
Yao mali wazuia.
308. Wamezidi khalifu,
Na mengineyo machafu,
Wala hawaoni hofu,
Maovu wafaharia.
309. Akili zao si tama,
Wamekuwa kama nyama,
Mizimuni watotama,
Sanamu kusujudia.
310. Kukicha wazidi hamu,
Kuhalalisha haramu,
Halali wailaumu,
Masanamu way'endea.
311. Mfano wana wachanga,
Wenye giza la ujinga,
Sanamu wameijenga,
Kwa tende kufinyangia.
312. Kisha wanaiabudu.
Na kuwa kama wadudu,
Wajianisi kwa shudu,
Uvundo wajivunia.
313. Sharia za taurati,
Vyema hawazifuati,
Wamejihimu kwa dhati,
Mabadiliko kutia.

Mfano huu tuliotoa umenukuliwa katika utenzi wenyewe. Labda mtunzi alitaka kuashiria kwamba maneno haya si yake, au kwa sababu zake mwenyewe amenukuu beti hizi. Au kuweka kinachosemwa katika muktadha fulani kama asemavyo Wamitila, (2008: 105)akimnukuu Sternberg.

kutia alama za mtajo katika usemi taarifa huru huwa ni kuweka kilichonukuliwa kwenye muktadha fulani tena kwa njia hii ni kuingilia matini-mweza asilia. Na kwamba kwa alama hizo huelekeza kwenye mtazamo fulani maalum ambao haupo bayana.

Usemi taarifa huru unapotumika huongeza ladha kwa maneno ya wahusika na kuleta mwingiliano kati ya wahusika na mwandishi. Aidha hukusudiwa kumpa msomaji hisia ya kumuonyesha mhusika mbele yake na vile vile usimulizi wa tukio, hali inayoleta mchanganyiko wa mimesia na daigesia. Mchanganyiko huu huipa kazi ya kifasihi sifa za kidrama na za usimulizi kwa wakati mmoja. Ni vyema kudokeza kuwa usemi taarifa huru una sifa zifuatazo; hauna matumizi ya kitegemezaji “kwamba” kama ilivyo kwa usemi wa taarifa, viashiria vya mahali (hapa, huku, humu n.k) havibadiliki na kuwa vya mbali kama vile; hapo, huko au humo. Pia vishazi viarifu huondolewa na maneno yanayohusishwa na usimulizi moja kwa moja hayatumiki.

Mawazo ya taarifa huru ni mtindo mwingine wa usemaji ambao huripoti mawazo ya muhusika sawia na usemi wa taarifa huru isipokuwa katika U.T.H uwasilishaji ni wa maneno yaliyotamkwa ilhali M.T.H msimulizi anaripoti mawazo ya mhusika. Mbinu hii Mtunzi hajaitumia katika uwasilishaji wake wa hadithi ya Nabii Isa.

3.6. Hitimisho

Tunaweza kusema kuwa, mtunzi wa *Utenzi wa Nabii Isa* ametumia mbinu au aina mbali mbali za uwasilishaji usemi japo zilizoshenehi utenzi huu ni zile za usemi halisi naza usemi wa taarifa. Nyingine hasa zinazohusiana na fikira ama mawazo kwa kiasi kidogo tu. Hata hivyo mtunzi anatuonyesha kwamba fikira za wahusika zaweza kuelezwaama kuonyeshwa kwa njia ya uandishi. Kwa kutumia aina hii ya uwasilishaji mtunzi anaonyesha kuwa njia ya kusawiri fikira za mhusika sharti ihusishwe na kuwepo kwa msimulizi maizi. Aidha ni kuonyesha jinsi uwasilishaji wa fikira za mhusika unazidi kuwa muhimu na wa thamani kuliko matamshi. Tukumbuke kwamba kinachotamkwa na mhusika ni dhahirisho ya kile alichokuwa akiwaza akilini mwake. Vile vile kwa kutumia usemi halisi na usemi halisi huru, mwandishi anatuonyesha namna wahusika wanavyoongea, hivi kwamba tungekuwepo tungewaona na kusikia sauti zao bila ya mwingiliano wa sauti ya msimulizi.

Kadhalika kwa kutumia njia hizi za uwasilishaji usemi (mawazo au kutamka) ni njia mojawapo ya mwandishi kubadili kiimbo, msimamo na masafa kati ya kinachosemwa na anayekisema au msemaji. Hivyo kubadili mbinu za usemaji na uwasilishaji mawazo hufanya mabadiliko kwa mitazamo ambayo matukio tofauti tofauti huangaliwa na kuamuliwa. Kwa mfano kabla Maryamu kumfahamu mjumbe wa Mungu, msimulizi ashafahamu kuwa huyu ni mjumbe wa Mungu ilhali Maryamu alimfahamu kama kijana mwenye nia mbaya kwake. Pia wakati Isa na wafuasi wake walitaka kuona ishara za Mungu. Isa alifahamu fika kwamba si jambo la mara moja na rahisi, lina dhiki na udhia ilhali wafuasi wake wadhani waendako wataziona ishara hizo kwa wepesi. Ndio maana walichoka na kumlalamikia Isa.

SURA YA NNE

MUUNDO, MTINDO NA MAUDHUI KATIKA *UTENZI WA NABII ISA*

4.1 UTANGULIZI

Katika sura hii tutajadili maana muhimu katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Baadhi ya masuala tumeyashughulikia ni maudhui kama yanavyojitokeza katika utenzi huu. Mtunzi wa utenzi huu ametunga kisa cha Nabii Isa (Yesu Kristu) kwa mtazamo wa Uislamu yeye mwenyewe akiwa mmjao wa jamii hii. Hivyo katika utenzi wake amejaribu kueleza masuala yanayoathiri jamii yake, ama kuwajaza au kuwaelimisha. Kwa kuwa ujumbe wa mwandishi aghalabu hubainika kupitia kwa maudhui, basi hatuna budi kuyatalii masuala haya aliyoyaeleza mtunzi wa *Utenzi wa Nabii Isa*. Baadhi ya maudhui yatakayoangaziwa ni pamoja na dini, ushujaa, miujiza, malezi, ndoa, maadili, sheria za torati, usaliti miongoni mwa nyingine. Aidha tutaeleza kwa muhtasari kisa chenyewe. Kadhalika tutafafanua muundo, mtindo na lugha kilingana na jinsi yalivyobainika katika sura zilizotangulia.

4.2 MUHTASARI WA KISA CHA NABII ISA

Utenzi wa Nabii Isa ulitungwa na Musa Mzenga. Utenzi huu ulichapishwa mwaka wa 1977. Ni utenzi unaohusu kisa cha mmojawapo wa manabii maarufu katika dini ya Uislamu – Nabii Isa, (ambaye katika dini ya Kikristo wanamuita Yesu au Kristu) hususan maisha yake kwa ujumla, tangu asili yake hadi hatima yake. Kisa hiki au hadithi hii haielezi moja kwa moja historia ya Nabii Isa, bali kinaanza kwa kueleza kuhusu babu na bibi yake Nabii Isa. Baada ya masimulizi ya babu na bibi yake Nabii Isa, Musa anaeleza pia kuzaliwa kwa mama yake Nabii Isa ambaye ni Maryamu binti Imrani. (Sehemu ya kwanza)

Baada ya maelezo haya, mtunzi anaeleza kisa chenyewe cha Nabii Isa hasa kuzaliwa kwake (sehemu 4), kupewa unabii (sehemu 7), misukosuko aliyoipata katika kazi yake ya kitume au unabii (kuanzia ubeti 352 ...), kupangiwa kuuawa na Mayahudi (sehemu ya 8) na mengineyo mengi yaliyompata. Kwa jumla ni kisa kinachohusu Nabii Isa tangu asili yake hadi mwisho wake.

Kwa jumla utenzi huu ambao ni wa kidini unaonyesha kisa chenye matendo mengi yenye uhalisia wa ajabu. Yaani matendo yanayofanyika katika utenzi huu yanaonekana ya ajabu ilhali kwa Wayahudi wenyewe ni jambo la kawaida, kwamba miujiza ndiyo inayowaimarisha katika imani yao au kwamba bila miujiza nivigumu wao kuamini. Na ni kisa cha kuisimua. Kinaeleza kuwa Maryamu mama yake Isa alizaliwa Imrani na mama yake. Hawa walikuwa wakiabudu msikitini kila mara. Baadaye Maryamu alichukuliwa na Mtume Zakaria ambaye alimlea na kumkuza katika mafunzo ya dini ya kiislamu. Ni wakati huu ndipo Maryamu alikutana na mjumbe wa Mungu akamvivia nguo iliyokuwa na nguvu za kimungu akapata mimba (ubeti 154 na 155) na baadaye akamzaa mtoto ambaye ndiye Nabii Isa.

Alipohitimu umri wa miaka thelathini Nabii Isa ndipo alianza kazi yake ya kitume kuongoza wana wa Israili (ubeti 298 – 300). Katika kazi hii haikuwa rahisi kwake kwani, alipata upinzani mkubwa kutoka kwa baadhi ya Mayahudi. Hata hivyo aliendelea na kazi yake ya kuhubiri na kutenda miujiza. Alifanya safari nyingi za karibu na mbali, aliwaonya Mayahudi dhidi ya kumfananisha Mola (ubeti 322), aliwakataza Waisraili dhidi ya uovu waliokuwa wakitenda na hata kuwajua kuhusu Mungu.

Haya yote wana wa Israeli hawakuyaona mambo haya kuwa yalitoka kwa Mola hivyo walitilia shaka unabii wake (352 – 357). Jambo hili lilileta upinzani mkali katika Israili na ndio uliokuwa mwanzo wa misikosuko yake katika maisha yake na hasa kwa kazi yake ya unabii. Kama tulivyotangulia kusema kwamba *Utenzi wa Nabii Isa* ni utenzi wa kidini, hasa ya Kiislamu. Hata hivyo utafiti huu hautajikita katika upande wa kidini wa utenzi huu bali utashughulikia usimulizi katika kisa hiki cha Nabii Isa katika utenzi huu ulioteuliwa, hususan kwa kuvichunguza vipengee vya wakati na uwasilishaji usemi kama ilivyo mada yetu.

4.3 MAUDHUI KATIKA UTENZI WA NABII ISA

Kwa mujibu wa Wamitila, (2003: 189) na Mohamed, (1995: 11) wanasema kuwa maudhui ni jumla ya masuala yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi yoyote ambayo huzuka katika uendelezaji na ukuaji wa dhamira ya kazi hiyo.

Tunakubaliana na maoni ya waandishi hawa kwa kusema kuwa maudhui pia ni fikira za mtunzi kulingana na muktadha fulani. Ni mambo yanayotokana na vile mtunzi anavyoikuza mada yake ambayo ndiyo hasa lengo lake kuu la kazi yake. Kadhalika tunaweza kusema kwamba wataalamu hawa – Wamitila na Mohamed wanatumia dhana hii ya maudhui kueleza kiwango cha maana cha kazi ya fasihi.

M'ngaruthi, (2008: 49), anasema kwamba hadithi inaweza kuwa na maudhui makuu na madogo.

Msimulizi anaweza kudhamiria kutuonya dhidi ya wivu. Katika dhamiri yake pakazuka maudhui kama vile kifo, iwapo mhusika atamuangamiza mwingine kutokana na wivu. Maudhui kama vile swala la dini namigogoro kazini na uongozi mbaya yanaweza kujitokeza katika masimulizi yayo hayo.”

4.3.1 Dini

Ni imani katika kuwepo kwa Mungu anayeaminiwa kuwa mwenye nguvu zaidi ya binadamu. Anayeumba na kuudhibiti ulimwengu. Aidha ni mfumo fulani wa imani na ibada zake. Ibada hizi za kidini ni kama vile: kuabudu Mungu, kusali, kuheshimu na kumtii huyu muumba. Hii inadhihirika katika tenzi nyingi ambazo ni za kidini hasa katika mwanzo au utangulizi wake. Tenzi hizi huanza kwa fomula ya kulitaja jina la Mungu. K. m*Utenzi wa Rasi 'IGHuli, Utenzi wa Amuri Ghuweni na Utenzi wa Barasisi* miongoni mwa nyingine. Tenzi hizi pia zinahusishwa na dini ya kiislamu.

Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, msimulizi amefuata fomula hii ya kulitaja jina la Mola. Jambo hili linatia uzito katika kazi hii ya utunzi ambayo inaonyesha kuwa bila msaada wa Mungu labda mtunzi hangeweza kufanikisha kazi yake. Hivyo utenzi huu katika dibaji yake, hasa kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa sita mtunzi anamuita Mola.

1. Kwa jina la Ramani,
Bwana mkubwa mbinguni,
Nakitia utenzini,
Kisa cha Isa Nabii.

2. Mungu unipe uwezo,
Wake yeye muongozo,
Nieleze maelezo,
Ya usawa nay a njia.
3. Kisa hiki ni adhimu,
Anija'alie Karimu,
Mambo yaliyo magumu,
Mema kunifunulia.
4. Nisimulie kwa hamu,
Itange hii ilimu,
Kisa cha biniadamu,
Isa alivyotukia.

Mwanzo wa kisa chenyewe unianza kwa kutaja jina la Mungu. (ubeti 9). Mwanzo huu unaonyesha jinsi mtunzi alivyo na imani thabiti katika dini yake, na pia anafanya kazi hii kwa kuongozwa na Mola. Aidha mwisho wa utenzi unamalizia kwa fomula ile ya kulitaja jina la Mola kwa kumshukuru (ubeti 822) na kuomba dua kwa ajili yake mwenyewe na wale watakaosoma utenzi huu (ubeti 827 - 834) akihimiza upendo kati ya waumini. Suala la sala limejitokeza sana katika utenzi huu. Katika jamii ya Waislamu, sala ina nafasi muhimu sana. Wanaamini kwamba yote yatukiayo kwa waumini huwa ni majibu ya sala. Haya yanadhihirika kwa mke wa Imrani. Baada ya kuomba kwa muda mola awajalie mtoto wa kiume Mungu anajibu dua yake japo kwa kumjalilia mtoto wa kike ambaye ni Maryamu, badala ya mtoto wa kiume.(ubeti wa 28 – 40). Katika hili Mungu amesawiriwa kuwa ndiye mpaji, na kwamba mtu hapati atakalo bali ajaliwalo na Mungu.

Shukrani kwa Mola pia ni jambo mojawapo muhimu sana katika jamii ya waislamu. Kwamba, unapojaliwa dua yako huna budi kumshukuru Mola. Baada ya mke wa Imrani kupata mtoto, alimshukuru Mola ingawa alipata mtoto wa kike kinyume na matarajio yake, (ubeti wa 41 – 45) ishara kwamba unapaswa kupokea na kushukuru kwa chochote kile akupacho Mola. Jambo jingine la dini linalojitokeza ni nafsi ya Mungu katika dini ya Kiislamu. Mungu ana nafasi kubwa katika dini ya kiislamu. Katika utenzi wa Nabii Isa msimulizi ameonyesha kuwa waislamu wanaamini kuwa kuna Mungu mmoja tu. (ubeti 347)

Humwambia ni mtume,
mushuka kwenu niseme,
Kuwajuza ufalume,
Kuwa Mngu ni mmoya.

Msimulizi pia ameeleza kuwa Mungu pekee ndiye wa kuabudiwa (ubeti 348). Aidha ni mwenye uwezo mkuu. Uwezo wa Mungu umeelezwa na kusifiwa kutoka mwanzo wa utenzi hadi mwisho wake. Mfano , (ubeti 411 - 412).

411. Na yeye akawajibu,
Uwezo wa kuwatibu,
Mola ni yangu sababu
Haya kunifikia.

412. Ni yeye mwenye uwezo,
Mola wa kuniongoza,
Wagonjwa nikawapoza,
Dhara kuwaepushia.

413. Mngu anenalo huwa,
Kombo au sawasawa,
Jambo hilo litakuwa,
Pasipo na kukawia.

Uwezo wa Mola pia unadhihirika kwa kumwezesha Maryamu kumzaa Isa bila kuonana na mume kimwili. (ubeti 177 – 192). Mbali na kuwa mwenye uwezo mkuu, Mungu amepewa sifa nyingi. Ni mwenye rehema (ubeti 47, 53, 118, 324), ni mwenye baraka (ubeti 180), ni mshindi (ubeti 145, 149), ni mpaji (ubeti 94,225), ni muumbaji (ubeti 33, 119, 231), ni mtawala (ubeti 264). Hizi na nyingine nyingi zinaashiria ukuu wa Mungu katika dini hii.

Sheria za dini pia zimedhihirika katika utenzi huu. Sheria hizi zimetajwa kama Taurati. Hizi ni kanuni, sheria au mafundisho yanayoongoza jamii, hususan dini ya Wayahudi. Torati kwa dini zote, kiislamu, kikristu na kiyahudi, inaaminiwa kuwa ilipewa Musa (siye mtunzi) na Mungu. Katika *Utenzi wa Nabii Isa* Mungu alimpa Mtume Musa torati (ubeti 664) ili iwaongoze Waisraili kufuata dini yao kikamilifu. Hivyo basi waliamini Mtume Musa tu ndiye aliyekuwa kiongozi aliyeweka msingi madhubuti wa imani yao na ndiye aliyewatendea miujiza.

- 357.” Imani hatutawaza,
Pasipo na miujiza,
Kama alivyotengeza,
Zamani Musa Nabii.
358. “Walionywa babu zetu,
Fimbo ya Musa kigutu,
Aridhini kuthubutu,
Nyoka kuwageukia.
359. “Ajabu hiyo yakini,
Kiifanya hadharahi,
Wazee wetu machoni,
Wenyewe kushuhudia.
360. “Tena akawaonyesha,
Babu zetu kuwatosha,
Mkono anaponyosha,
Mara yai huawia.
361. “Mitupu mikono yake,
Chochote asikishike,
Kwa Musa ibainike,
Miujiza ya Nabia.
363. “Kwani Musa uhodari,
Mkono kutuashiri,
Kofi lake huja nuri,
Anga kama shamsia.

4.3.2 Usaliti

Ni utoaji wa siri ya mtu kwa mtu mwingine iliakamatwe. Pia usaliti ni kuungana na adui ili kuweka maisha ya unayemthamini katika hatari. Usaliti umedhihirika katika *Utenzi wa Nabii Isa* pale ambapo mmoja kati ya wafuasi wa Nabii Isa ambaye waliishi pamoja na kufanya kazi pamoja, mtu wake wa karibu (mfuasi wa Nabii Isa) anadanganyika kwa tamaa ya kupata cheo na mambo mema katika maisha yake, akafichua siri ya alikojificha Nabii Isa.

786. Ilani ilipofika
Wanafunzi kipulika,
Mmoja kahadaika,
Kwa tamaa kumwingia.

787. Akawa yuko tayari,
Kuwapokea asikari,
Hadi maficho ya siri,
Alipo wao Nabii.
788. Hivyo akawadokeza,
Asikari kuwe'leza,
Kuwa atawaongoza,
Isa alipofikia.
789. Naye huyu matawala,
Kupata hii risala,
Kwa furaha hakulala,
Kasha akakusudia.
790. Kuzidiwa ni shauku,
Wao na huyo mdaku,
Wakaondoka usiku,
Khaini kuonya njia

Mpango huu ulikuwa wakishamkamata Nabii Isa, wamuuwe. Jambo ambalo Mola hakuliliridhia (ubeti 791). Kwa hivyo, Mungu akabadili sura ya Nabii Isa, akaipa msaliti yule (ubeti 795). Basi badala ya Nabii Isa kukamatwa akakamatwa yeye, akateswa, akapelekwa msalabani na kusulubiwa. (ubeti 801 na 802). Hivyo ndivyo Mola alivyomuokoa Nabii wake Rasuli.

4.3.3 Dhuluma.

Ni kuonea mtu, ni kumnyima mtu haki yake au kumfanyia mtu tendo lisilo haki. Ni kutaabisha, kutesa au kumthakilisha mtu. Kwanza kabisa dhuluma katika *Utenzi wa Nabii Isa* inabainika kupitia kwa wakuu wa Mayahudi, viongozi wa dini, maimamu na makuhani. Hawa wanawanyanya watu. Fukara na masikini na waumini. Hawa huchukuwa zaka na sadaka zitolewazo na waumini na kuzitumia kwa mahitaji yao. Wake na vijana wao pia hudhulumu raia. Aidha huiba mali misikitini, kuwapa wanabiashara na wakulima hasara na kupindua sharia ili ziwafae wao (ubeti 650 - 656).

Nabii Isa mwenyewe hakusazwa katika dhuluma zilizokuwa zikifanyika Israili. Watu aliokinzana nao walimshuhudia uongo. Hasa walimu wa dini na makuhani walishikwa na wasiwasi walipoona Nabii Isa akipata umaarufu na idadi ya wafuasi wake kuongezeka. Hivyo waliazimu kumuangamiza kwa kusema uongo kwa wakuu wa Roma kwamba

anapotosha imani ya watu, Isa ni muasi, hafuati sharia, anakashifu sharia kwamba hazifai, anataka kutawala, na mengi waliyomshuhudia. (ubeti 763 – 778) Mbali na uongo aliozushiwa Nabii Isa alitusiwa na mama yake pia. (ubeti 672 - 675). Japo haya, yote Nabii Isa aliyavumilia kwa saburi. Ni kweli kwamba mashujaa wengi hukumbana na matatizo mengi katika maisha yao. Haya yamedhihirika katika maisha ya Nabii Isa katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Jambo hili basi linatuashiria kwamba kuna maudhui ya ushujaa katika utenzi huu.

4.3.4 Ushujaa.

Ushujaa ni hali ya kutokuwa na woga, au hali ya kuwa hodari. TUKI (2013) inaeleza kuwa ushujaa ni hali ya moyo thabiti, ujasiri au ghamidha. Ushujaa ni hali muhimu kwa binadamu. Ni hali inayomfanya mtu kukabiliana na jambo katika maisha ili kujinasua katika hali au jambo linaloumiza aidha kibinafsi au kijamii. Mtu aliye na hali hii hujulikana kama shujaa au jagina. Ili shujaa apate cheo katika jamii lazima akipigania dhidi ya wapinzani au maadui wake.

(Gathira, 2015) akiwanukuu Njogu na Chimera (1999), anasema hakuna shujaa yeyote ulimwenguni asiyekuwa na maadui. Hata hivyo japo huwa na maadui, hakosi watu wanaompenda. Hivyo basi shujaa huwa na wafuasi. Kwa ujumla maisha ya shujaa huwa ya miujiza na yaliyosheheni matatizo na hufikia kikomo pale ambapo lengo lake hutimia. Sifa hizi za kijagina zinadhihirika katika maisha ya Nabii Isa katika utenzi wa Nabii Isa.

Kuzaliwa kwa Nabii Isa kulikuwa kwa miujiza. Kabla mama yake Bi. Maryamu kuolewa, akiwa bado binti mdogo malaika alimjia kumpa ujumbe kutoka kwa Mola kwamba atamzaa mtoto wa kiume (Ubeti 128 – 137). Bila Bi Maryamu kuonana na mwanamume kimwili alipata mimba kwa kuviviwa nguo na malaika (ubeti 155, 165, 1168 – 178). Wakati ulipotimia wa mtoto kuzaliwa, Bi. Maryamu aliondoka ili asionekane. La ajabu ni kwamba katika umri wake mdogo Bi. Maryamu aliweza kujifungua bila usaidizi wa wakunga. Mwana alimzaa peke yake chini ya mtende mbali na watu. Musa (mtunzi) anaeleza kwamba Bi. Maryamu hakusumbuka wala kutumia nguvu wakati wa kumzaa Nabii Isa (ubeti 186 - 190).

Sifa nyingine ya jagina ni kuwa na akili iliyojevuka na kufanya mambo makuu yaliyozidi umri wake. Nabii Isa alianza kuongea mara tu alipozaliwa kwa kumliwaza mama yake alipomuona akiwa na shaka na hofu kwa yale yatakayompata atakapogunduliwa kwamba

yuna mtoto nje ya ndoa (ubeti 191 – 205). Pia katika sehemu ya tano ya utenzi huu, Nabii Isa anaonyesha upevu wake katika umri mchanga anapomtetea mama yake na ghadhabu ya watu waliomshambua kwa maswali kuhusu kuzaliwa kwake (Nabii Isa). Aidha mafundisho aliyofunza Nabii Isa ni dhihirisho ya upevu wa akili yake. Ni mafundisho ambayo wengi waliyaajabia, ikidaiwa kwamba Nabii Isa hakuwa na kisomo cha juu.

528.” Ni kwa hayo matukio,
Ya Isa mafanikio,
Mno ya maajabio,
Watu alowafanyia.

544. kwa maneno ya kutimu,
Fasaha na ilimu,
Kutujuza tufahamu,
Kuwa yeye ni Nabia.

546. Ni mwingi wa taaluma,
Wala sana hokusoma,
Na mambo chungu nzima,
Yeye yanamuelea.

Katika kutekeleza kazi yake ya kitume haikuwa rahisi. Nabii Isa alikumbana na upinzani, mateso, dhuluma, kukataliwa, kusalitiwa, kusingiziwa na hata kupangiwa njama ya kuuawa kutoka kwa wapinzani wake. (ubeti 398 -402, 774 – 778, 786 – 790). Hata hivyo, japo alikumbana na haya yote, hakukosa wafuasi. Nabii Isa alipata kikosi cha waliomuamini.

535. Siku moja ikatuka,
Idadi kukutanika,
Watu wa mbili tabaka,
Ya Isa wahadithia.

Katika sehemu ya 12 na 13 ya utenzi huu, Nabii Isa anonyeshwa akiwa na wanafunzi wake, dalili ya kuwa katika kazi yake ya kitume hakuwa peke yake, alipata wafuasi waliomwamini, kusafiri pamoja na kutenda kazi pamoja. Haya na megine mengi katika maisha ya Nabii Isa yanamdhihirisha kwamba alikuwa shujaa.

4.3.5 Miujiza

Utenzi wa Nabii Isa umesheheni matendo ya kimiujiza aliyoyafanya Nabii Isa. Mgogoro kinzani ulizuka. Kulikuwa na wale waliomwamini Nabii Isa na wale waliopinga unabii wake.

Wale ambao hawakumuamini Nabii Isa walitaka kuonyeshwa miujiza ili waweze kumwamini (ubeti 357). Jambo la kwanza alilofanya Nabii Isa, ni kumtaja bwana mmoja chakula alichokula asubuhi na jioni, maji aliyotumia, hela alizokuwa nazo mfukoni na akiba aliyojiwekea nyumbani. Na haya yote mwenye kuuliza alikiri kwamba ni ukweli. (ubeti 380 – 395). Baada ya kuona alidhihirisha Nabii Isa kuna wachache walimwamini, lakini bado kunalo kundi ambalo halikukubali haya. Hivyo walizidi kudai kutendewa miujiza mingine.

Nabii Isa aliwafanya vipofu kuona (ubeti 422) na kuponya wagonjwa (ubeti 424 – 427). Aidha aliumba ndege kwa kufinyanga udongo kisha akawavuvia wakawa hai wakapeperuka angani (ubeti 466 – 473). Suala jingine la kimujiza alilolifanya Nabii Isa ni lile la ufufuo. Nabii Isa alimfufua mtu mmoja waliyemtaka. Kisha baada ya kuzungumza na watu alirudi kuwa mfu tena. (ubeti 508 – 518). Hata hivyo, baada ya miujiza hii yote bado walikuwepo na watu ambao hawakumkubali unabii wake. Na hivyo kumpangia njama ya kumuangamiza. Jambo ambalo Mwenyezi Mungu hakulikubali. Akatenda muujiza yeye mwenyewe wa kumgeuza sura mfuasi wa Nabii Isa aliyedhamiria kumsaliti kwa mayahudi, akachukuwa sura ya Nabii Isa na hivyo badala ya kuuawa Nabii Isa bahili huyu akauawa na mayahudi (ubeti 795 – 803).

Mbali na miujiza aliyofanya Nabii Isa, ipo miujiza inayodhirika katika utenzi huu. Kule kuzaliwa kwa Nabii Isa kulikuwa kwa miujiza – bila baba. Mama yake Maryamu binti Imrani alimzaa pasi kuonana kimwili na mwanamume. (ubeti 588). Kwa jumla utenzi huu umejaa miujiza toka mwanzo hadi mwisho. Wamitila, (2003, uk. 274) ameyaita matendo haya matendo ya kiuhalisia ajabu.

4.3.6 Uvumilivu

Maudhui ya uvumilivu yamejitokeza katika (ubeti 672 – 675) katika utenzi huu pale ambapo Nabii Isa anatukanwa yeye mwenyewe na ya uchungu zaidi kutukaniwa mama yake pasi kujibu au kulipiza lolote. Pia masumbuko aliyoyapata katika kutekeleza utume wake, safari alizozifanya ambazo zilikuwa za dhiki na taabu nyingi, kukosa chakula, kujaribiwa na Mayahudi kwa kutenda miujiza mingi ambayo hata baada ya miujiza hiyo hawakukubaliana naye kuwa yeye ni nabii wa Mola. n.k. Haya yote Nabii Isa aliyavumilia mradi kutimiza aliyotumwa na Mola wake. Uvumilivu huu unaashiria maudhui mengine ya maadili na

malezi. Kwamba mtu aliyepata malezi mazuri huwa na maadili. Uvumilivu ikiwa sifa mojawapo ya dhana hizi mbili.

4.3.7 Malezi na maadili

Malezi ni namna ya kumkuza mtoto kwa kufuata utaratibu fulani unaokubalika katika jamii. Malezi hujumuisha mambo yote ambayo mtu au mtoto anapaswa kupewa na mlezi wake kwa ukuaji wake. Aidha ni tabia na mwenendo, uangalizi, mafunzo na yale yote yanayomkuza mtu au mtoto. Ni katika malezi ndipo maadili hupatikana. Hivyo tunaweza kusema kwamba maadili ni kipengee mojawapo katika malezi na hasa malezi mema. Nayo maadili nimwenendo mwema, onyo au mafundisho yatolewayo kwa njia ya hadithi au shairi kwa nia ya kufundisha; mafundisho mazuri. Basi kulingana na madai haya, yeyote asiyepata malezi haya au kulelewa kwa utaratibu unaostahiki huonekana mtovu wa nidhamu na asiye na maadili. Mara nyingi jukumu hili huachiwa wanawake hasa katika jamii zetu za kiasia, ikichukuliwa kuwa mwanamke (mama) ndiye aliyekaribu zaidi na watoto katika umri wao mdogo.

Utenzi wa Nabii Isa ulio utenzi wa kidini hususan ya kiislamu malezi yamepewa kipaumbele ikizingatiwa kwamba dini ya kiislamu inatilia mkazo na maanani maadili na hasa malezi ya watoto na kuhimiza wazazi kuwalea watoto katika maadili na kuwapa mafundisho hasa ya dini. Malezi katika *Utenzi wa Nabii Isa* yanaanzia kwa Imrani na mkewe wakimlea Maryamu katika njia nzuri na kwa msingi wa dini. Baadaye Maryamu anachukuliwa na mtume Zakaria ambaye anaendeleza malezi haya. Maryamu anaonyesha uadilifu kwa kufuata sharia na kanuni za dini aliyofunzwa na kukuzwa. (ubeti 56 - 70) uadilifu huu unaendelezwa na Maryamu kwa kumlea Nabii Isa ambaye anaonyesha uadilifu wake katika kuendeleza dini kwa kuhubiri na yote aliyoagizwa na Mungu kuyatenda.

Tofauti ya malezi ya Maryamu na ya Nabii Isa ni kuwa malezi ya Maryamu yalikuwa ya jamii nzima. (ubeti 61) baada ya mama yake kuaga dunia wengi katika jamii walitaka kumlea Maryamu, lakini kura inamwangukia Mtume zakaria ya kumlea Maryam (ubeti 67 – 81). Isa kwa upande wake, alilelewa na mama yake pekee tangu akiwa tumboni hadi kuzaliwa kwake na hata ujana wake, jamii ikimlaumu Maryamu kwamba alipata mimba nje ya ndoa. Jambo ambalo halikukubaliwa katika jamii yake. (ubeti 282 – 297). Na hasa

wakizingatia maadili ya dini yao ya Kiislamu. Hivyo kuonyesha jinsi jamii hii ilivyothamini na kuipa umuhimu ndoa.

4.3.8 Ndoa

Ndoa ni makubaliano rasmi kati ya mwanamume na mwanamke kuishi pamoja kama mume mke. Ndoa ni asasi iliyoasisiwa na Mungu mwenyewe. Katika Biblia Takatifu tunasoma kwamba Mungu aliumba mume na mke (Adamu na Hawa) akawaweka katika shamba la Edeni. (Mwanzo 2:7,18,21 – 24). Hii ndio iliyokuwa ndoa ya kwanza iliyofunga na Mungu mwenyewe kuonyesha jinsi ilivyo muhimu. Muungano wa wawili hawa – mume na mke, ndio unaoendeleza na kukuza jamii na ndio msingi wa familia. Ni kutokana na ndoa watoto huzaliwa hivyo kuendeleza jamii. Vilevile katika dini ya kiislamu ndoa imechukuliwa kwa uzito na umuhimu sana. Ndiyo maana Bi. Maryamu anapoonekana na mtoto asiyejulikani baba yake inaibua taharuki na maswali mengi katika jamii yake (ubeti 242 - 258). Wasijue kwamba ni Mola mwenyewe ameamuru hili litendeke kwa kudhura zake. Maryamu anaonekana mvunja sharia, mchafu, mpotevu n.k.

Maudhui haya ya ndoa yanaonekana kwa Imrani na mkewe walioweka ndoa yao katika msingi wa dini hasa ya kiislamu kama tujuavyo huu ni utenzi wa kidini hasa ya kiislamu. Katika ndoa yao waliambatana katika kila jambo walilolitenda la kiimani kwa mfano kuenda msikitini pamoja, Imrani ambaye alikuwa imamu wa dini walisimamia ibada na kuabudu pamoja na mkewe n.k (ubeti 21 - 22). Mtume Zakaria pia anaendeleza maudhui haya ya ndoa kwa kuishi na mkewe wakimlea Maryamu katika misingi ya kidini. Hii inaonyesha wazi jinsi maudhui ya ndoa yalivyoshamiri katika utenzi huu wa Nabii Isa na jinsi ilivyo muhimu hususan katika dini ya kiislamu ambayo pia ndiyo imani ya mtunzi wa utenzi huu.

4.4.1 MUUNDO

Wamitila (2003: 153) anaeleza kuwa muundo ni dhana inayotumiwa kueleza jumla ya uhusiano uliopo kati ya visehemu mbali mbali vinavyounda kitu cha ujumla. Anaendelea kusema kuwa muundo hutumika kueleza sifa za nje zinazoipa kazi ya fasihi sura inayotambulika. Muundo hauhusikani na elementi zinasodhihirika kijuujuu tu ,kunazo elementi za kimuundo ambazo hazionekani kwa kuitazama kazi ya fasihi. Elementi hizi hutambulikana kazi inaposomwa. Madai haya yameweza kuzua dhana mbili za muundo –

muundo wa ndani na muundo wa nje. Muundo wa ndani hauonekani kwa macho isipokuwa kwa kuisoma kazi yenyewe. Vipengee vya aina hii ya muundo ni pamoja na usimulizi, matumizi ya lugha, wakati na msuko. Nazo sifa za muundo wa nje hujumuisha vina, urefu wa kazi, idadi ya mishororo, vipande katika mshororo, idadi ya mizani n.k.

Mohamed (1995: 5), anasema kuwa muundo ni hatua ya kushikamanisha vipengee au vitu mbalimbali kwa utaratibu au mfumo na ubingwa fulani ili kuleta umbo la kitu fulani. Anaeleza kuwa,

Tunapozungumzia muundo, tunatarajiwa kushughulikia
kitu kimoja katika kuchunguza jinsi kitu hicho
kilivyoshikamanishwa na vitu vingine katika utaratibu
uliotumiwa hatimaye kupata umbo fulani.

The New Princeton Encyclopedia of Poetry and Poetics, Brogan, (1993) inaeleza kwamba muundo ni istilahi ambayo inatumika kwa mapana katika fasihi licha ya kuwa tata. Hii ni kwasababu inatumiwa kwa njia tofauti tofauti katika fasihi. Kwa sababu ya sifa hii iliyotajwa, Ensaiiklopedia inaendelea kueleza kuwa,

Kwa wakati mmoja inamaanisha mambo
madogo madogo katikamatini, wakati mwingine
umbo la utungo Fulani na hata pia sifa za kazi
fulani, ama hata kuwa na maana nyingine zaidi
katika kazi ya mtaalamu mmoja. (uk. 420)

Hata hivyo, kwa kufuata maelezo haya ya ensaiiklopida, utafiti huu umepata fasili ya istilahi hii ya muundo kwa jinsi itakavyotumika na kuonekana muhimu kwa utafiti huu. Hivyo basi kwa kuyarejelea maelezo haya muundo inahusisha mtindo, umbo na desturi za aina fulani ya tungo. Muundo umejumuisha sifa zinazodhihirika kwa kutazama utungo. Sifa hizi wataalamu wameziita sifa za kiarudhi.

Abedi, (1954) katika utangulizi wake anasema kwamba shairi au utenzi ni wimbo, hivyo kama ni wimbo lazima uimbike na kama hauimbiki basi hauna maana. Anaendelea kusema kwamba zipo kanuni ambazo sharti zifuatwe katika utenzi wa shairi lolote. Kanuni hizi ni za jadi zilizopokezwa na watunzi wa jadi. Ni kanuni hizi zinatupa muundo wa utenzi.

Utenzi wa Nabii Isa kama tenzi nyingine za Waswahili umetungwa kufuata kanuni hizi. Lau usingefuata kanuni hizi ungeordheshwa katika aina ya mashairi guni. Kanuni hizi ambazo Abedi anazitaja ni pamoja na urari wa vina, idadi ya mizani, kibwagizo, beti n.k. Wataalamu wameziita kanuni hizi arudhi. Kwa kufuata kanuni hizi *Utenzi wa Nabii Isa* unajidhihirisha kuwa ni utenzi wa jadi au wa kimapokeo. Katika sehemu hii tumetumia sana Abedi katika maelezo ya istilahi au kanuni hizi za utungaji wa mashairi ya jadi.

4.4.1.1 Mizani.

Abedi, (1954) anaeleza mizani kuwa ni silabi au tamko katika shairi. Mizani ndizo hutumika kama kipimo cha urefu wa mstari katika shairi. Kwa kuzingatia kigezo hiki cha mizani tunapata aina tofauti tofauti za tenzi. Kama anavyozitaja Abedi kuna tenzi za mizani 8, za mizani 11 na za mizani 6. Utenzi wa Nabii Isa ni utenzi wenye mizani nane (8) katika kila msitari. Mtunzi amefuata kanuni hii bila kuikiuka mahali popote katika utenzi huu na bila kupoteza ujumbe aliodyhamiria kuutoa. Jambo hili limefanyika kiufundi na kuonyesha ubingwa wake katika utunzi wake.

3. Ki – sa – hi – ki – ni – a – dhi – mu,

1 2 3 4 5 6 7 8

A – ni – ja – ‘li – e – ka – ri – mu,

1 2 3 4 5 6 7 8

Ma – mbo – ya – li – yo – ma – gu – mu,

1 2 3 4 5 6 7 8

Me – ma – ku – ni – fu – nu – li – a.

1 2 3 4 5 6 7 8

327. Ha – ku – wa – mwe – nye – u – nda – ni,

1 2 3 4 5 6 7 8

U – ki – mwa – na – u – ku – ngu – ni,

1 2 3 4 5 6 7 8

Mu – ku – ta – na – po – nji – a – ni,

1 2 3 4 5 6 7 8

Sa – la – mu – hu – ta – ngu – li – a.

1 2 3 4 5 6 7 8

Mifano hiyo hapo juu inadhihirisha wazi kwamba mtunzi amefuata kanuni hii ya mizani nane katika kila msitari hivyo kuweka desturi ya utunzi wa tenzi za Waswahili.

4.4.1.2 Vina

Hizi silabi au tamko la namna moja linalopatikana baada ya idadi fulani ya mizani katika msitari wa shairi. Mizani hii hufanana katika mistari mitatu ya kwanza ya kila ubeti isipokuwa msitari wa mwisho huwa tofauti. *Utenzi wa Nabii Isa* una urari huu wa vina mwishoni mwa kila ubeti katika mistari mitatu ya kwanza. Kina hiki hubadilika katika mistari wa nne ambacho kimerudiwa katika beti zote za utenzi mzima. Kina hiki ambacho kimejitokeza katika mwisho wa mistari wa nne katika kila ubeti unajulikana kama **bahari**. Bahari inaashiria mwisho wa ubeti na pia kuonyesha kwamba ni mwanzo wa ubeti mwingine. Mizani hii pia inaleta mdundo na mvuto maalum katika kughani utenzi ambayo ni sifa mojawapo ya tenzi za Waswahili. Ifuatayo ni mifano ya beti katika utenzi wa Nabii Isa inayodhihirisha haya.

298. Hivyo bin Maryamu,
Katika yake kaumu,
Thalathini akatimu,
Miaka alofikia

445. Wafanyiwe miujiza,
Zaidi hiyo ya kwanza,
Ndipo watapendekeza,
La kumtwii nabia.

671. Isa amekuta adha,
Na visa kadha wa kadha,
Ela hivi ni baadha,
Ambavyo mewatajia.

4.4.1.3 Mishororo

Yapo mashairi ya aina nyingi. Mashairi yaliyozoeleka au kujulikana sana ni mashairi yaliyo na mishororo minne katika kila ubeti. wengi wa watunzi wa tenzi wamechukuwa mfumo huu wa mishororo minne katika kila ubeti wa utenzi. Mtunzi wa *Utenzi wa Nabii Isa* pia amechukua muundo huu wa mishororo mine katika kila ubeti. Pengine kulingana na ujumbe aliotaka kuwasilisha ama kwa sababu ndio muundo ulio maarufu.

Ufuatao ni mifano ya mistari au mishororo katika ubeti.

608. 1. Tena lipo jambo gani,
2. Lilo geni duniani,
3. Alipendalo Manani,
4. Mjawe kumja'lia.

4.4.4 Beti

Kama tenzi nyingine zozote za Waswahili zilivyo na beti nyingi, utenzi wa Nabii Isa pia una beti nyingi. Ni utenzi uliotungwa kwa beti 834. Pengine ni kwa sababu ya urefu wa kisa alichotaka kusimulia mtunzi na kilichohitaji beti nyingi ili kukamilika ama kwa kufuta kanuni ya kwamba utenzi lazima uwe mrefu, japo jambo la urefu bado halijatatuliwa na watafiti kwamba ni urefi wa kiasi gani hasa tukizingati idadi ya beti. Mfano tulioutoa hapo juu kuhusu idadi ya mishororo katika kila ubeti yanadhihirisha mpangilio wa beti katika utenzi huu.

2.4.1.5 Muundo wa utatu

Utenzi wa Nabii Isa umegawika katika sehemu tatu kuu; fomula tangulizi au dibaji, mwili na fomula tamati. Fomula tangulizi pia dibaji au utangulizi ni sehemu inayoitangulia simulizi yenyewe. Tenzi za Kiswahili zina miundo ya kifomula. Ni sharti zianze kwa kumtaja au kumuomba Mungu. Katika mila na desturi za dini ya Kiislamu hakuna jambo lolote lianzalo bila kumuomba Mungu. Kwao hili si dini tu bali moja wapo ya vipengee vya maisha yao. Vivyo hivyo hata tungo zao ni sharti zianze kwa jambo hili. Mtunzi ameanza katika ubeti wa kwanza kwa kumuita Mungu na kumsifu au kumtukuza .

“kwa jina la Rahamani,
Bwana mkubwa mbinguni,

Katika beti zote katika dibaji yake hasa kuanzia ubeti wa pili wa sita, mtunzi amejishusha na kuonyesha kwamba kazi hii bila uongozi wa Jalali haitafaulu. Kwa hivyo anamuomba Mola amuongoze katika utunzi wake na kuufanikisha. Aidha anamuomba Mola Baraka ya kutunga kisa kitakachowavutia na kuwafaa watu hasa watakaosoma utenzi huo. Utangulizi huu ni muhimu pia kwa sababu mbali na kumuomba Mola amuongoze, mtunzi ametujulisha ni kisa cha nani anachotaka kuhadithia hivyo kuwapa hamu hadhira yake ya kuusoma utenzi huu. Hapa chini ni dibaji ya mtunzi (ubeti 1 – 6) kuthibitisha madai haya.

1. Kwa jina la Rahamani,
Bwana mkubwa mbinguni,
Nakitia utenzini ,
Kisa cha Isa Nabia.
2. Mungu anipe uwezo,
Wake yeye muongozo,
Nieleze maelezo,
Ya usawa nay a njia.
3. Kisa hiki ni adhimu,
Anija'lie Karima,
Mambo yaliyo mangumu,
Mema kunifunulia.
4. Nisimulie kwa hamu,
Itange hii ilimu,
Kisa cha binadamu,
Isa alivyotukia.
5. Kupanda na kushukani,
Kwa ridha yake Manani,
Awe wangu usukani,
Njia kuniongozea.

Sehemu ya pili ya utenzi ni mwili. Hii ndiyo sehemu kuu katika kazi yoyote ya fasihi. Ndiyo inayobeba simulizi lote ambalo msimulizi anasimulia. Nisehemu iliyo kati ya utangulizi na hitimisho.

Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, sehemu hii ndiyo iliyo na maelezo yote ya kisa cha Nabii Isa tangu asili yake hadi hatima yake. Sehemu hii imegawika katika sehemu nyingine ndogondogo kumi na nne. Sehemu ya kwanza inazungumzia juu ya kuzaliwa bi Maryamu binti Imrani ambaye ni mama wa Nabii Isa. Ya pili inaeleza jinsi Bi. Maryamu alivyochukuliwa na mtume Zakaria na kumlea pamoja na mkewe. Hii inafuatwa na sehemu ianayoelezea kukutana kwa Maryamu na malaika wa Mungu aliyemletea ujumbe wa kwamba atachukuwa mimba kwa uwezo wa Jalali na kumzaa mtoto wa kiume - Nabii Isa ambaye ndiye mhusika mkuu katika utenzi huu. Baada ya maelezo haya inafuata kuzaliwa kwa Nabii Isa mwenyewe. Sehemu ya tano ni maelezo ya jinsi Maryamu alivyorudi kwao akiwa na mtoto wake. Safari hii haikuwa rahisi kwake maryamu, alikuwa na hofu nyingi akijua kuwa

hatapokelewa vema hasa kwa kupata mtoto nje ya ndoa, watu wa kwao walidhani kuwa amekiuka sharia.

Malezi ya Nabii Isa yanafuata sehemu hii. Malezi ambayo aliyapata kutoka kwa mama yake. Baada ya kuhitimu umri miaka thelathini Nabii Isa anapewa kipawa cha unabii ambayo ndiyo kazi yake mahsusi Mola aliyomletea duniani. Mara tu baada ya kupewa kipawa hiki na Mwenyezi Mungu Nabii Isa anaanza kazi yake kwa kuhubiri ambayo haikuwa rahisi kwake kwa sababu watu - mayahudi hawakuyaridhia. Kwa sababu hawakuyapokea mahubiri yake Wayahudi walidai wafanyiwe miujiza ili kumkubalia asemayo. Akafanya miujiza mingi kwa uvumilivu. Hata baada ya miujiza mingi aliyoifanya hawakukubali mafundisho yake hivyo kukazuka ukinzani kati ya wana wa Israili, kukawa na makundi mawili, kundi lililomuamini Nabii Isa na lile ambalo halikumuamini. Hili halikumzuia Nabii Isa kufanya kazi yake hivyo aliendelea kuhubiri. Hii ikitukamilishia sehemu ya kumi na moja. Sehemu ya kumi na mbili ni maelezo ya Nabii Isa na wanafunzi wake wakienda huku na huku wakifanya kazi ya kuwafundisha watu kumjua Mungu na kuwaonya dhidi ya njia zisizomuelekea Mungu. Ni katika sehemu hii Nabii Isa na wanafunzi wake wanaondoka mjini kwa kusudi la kuziangalia alama za Mungu anavyoipa dunia uhai (ubeti 700). Baada ya kukamilisha jambo hili Nabii Isa na wanafunzi wanarudi mjini (sehemu ya 13) na mwisho kabisa ni sehemu ambayo Mayahudi wanampangia njama Nabii Isa ili kumuua, jambo ambalo halifaulu kwani Mungu hakuliridhia na hivyo kumuepusha na mikono ya watu waovu.

Sehemu kuu ya tatu ni fomula tamatisho au sehemu ya hitimisho. Hii ndiyo sehemu ya mwisho na ambayo huja baada ya mwili wa kazi yote. Sehemu hii hufunga kazi ya fasihi au utenzi na hususan utenzi wa kidini. Kama tulivyotangulia kusema tenzi za Waswahili na hasa za dini ukiwemo utenzi wa Nabii Isa una fomula maalumu ya kuanza na kumaliza, utenzi wa Nabii Isa umemalizika kwa kumshukuru Mungu, msimulizi pia anadhihirisha wazi kwamba amemaliza utungo wake.

822. Mtungaji nashukuru,

Kwa haya nilodhukuru,
Nikaweza jikusuru,
Kisa kuwahadithia.

823. Tokea mwanzo wa kisa,
Juhudi nimejipasa,
Utenzi wa Bwana Isa,
Kisa kuwamalizia.

Katika sehemu hii mtunzi anaomba kwa unyenyekevu kuelezwa marekebicho iwapo hadhira yake itapata makosa yoyote katika utunzi wake. Aidha anaomba dua ya hifadhi kwa Mola kwa ajili ya jamii yake ya waislamu. Anamuomba Mungu awabariki na kuwajalia mahitaji yao na kuwaepusha na watu waovu. Mtunzi anawanasihi jamii yake waishi wakipendana na kujiepusha na jambo lolote litakalawatenganisha. Mwisho kabisa anamalizia na dua yake kwa fomula ile ile ya kumaliza dua katika swala za kiislamu. Ishara kwamba si utungo tu anamalizia bali ni dua kamili anayotoa kwa Mungu aliyemuwezesha kukamilisha kazi yake. (ubeti 827 - 834).

Mbali na sehemu hizi kuu tatu ambazo ni tulizozieleza hapo juu, *Utenzi wa Nabii Isa* kwa jumla umegawanyika katika vijisehemu vingine vidogo vidogo ambavyo vimejenga utenzi mzima. Kwa jumla utenzi huu una vijisehemu kumi na vitano pamoja na dibaji. Sehemu hizi zimeshaelezewa hapo juu.

4.4.2. Mtindo

Wamitila, (2003: 145) anaeleza kuwa mtindo ni jinsi msimulizi fulani anavyojieleza katika kazi yake. Maelezo ya Wamitila yanalandana na maelezo ya *The New Princeton Encyclopedia* (uk.1226) kwamba, kwa mtazamo wa uandishi, mtindo huonyesha upekee wa mwandishi katika kujieleza katika kazi yake. Hii inaonyesha kwamba mtindo huwa tofauti. Yaani kila mwandishi huwa na mtindo wake wa kueleza ujumbe wake katika kazi yake ya kifasihi. kwa kutumia maelezo haya tutaagalia jinsi Musa Mzenga alivyojieleza au ni mtindo gani anaoutumia kuieleza hadithi ya Nabii Isa katika *Utenzi wa Nabii Isa*.

4.4.2.1 Usimulizi

Usimulizi ni uelezaji wa matukio katika hadithi. Wamitila (2003: 325). Mawazo haya yanalingana ya mawazo ya Burundi na wenzake, (2014: 74) wakimnukuu Kanar (2001) wanasema kuwa usimulizi ni mtindo mpangilio unaotumiwa na mwandishi katika hotuba, na utanzu wa kibunilizi kuelezea matukio. Mtaalamu mwingine anayetoa fasili ya usimulizi ni

Mohochi, (2000: 50) akimnukuu Attenbernd na Lewis (1963), anasema kwamba usimulizi ni mkabala unaotwezesha kuyatazama yanayozungumzwa katika kazi ya fasihi.

Kwa kutumia mawazo ya wataalamu hawa tunaweza kusema kuwa usimulizi ni namna ambavyo mwandishi anatumia mbinu za usimulizi katika kuelezea matukio kwa jinsi alivyopanga katika hadithi yake. Kuna aina mbali mbali za usimulizi, Wamitila, (2003: 325 – 8) anaainisha usimulizi kama ifuatavyo, usimulizi anuwai, usimulizi ngazi, usimulizi maizi, usimulizi penyezi au dukizi, usimulizi sawia, usimulizi tangulizi, usimuliziki-itimamu, usimulizi ki-utendi, usimulizi wa kirejeshi, usimulizi wa kiutomaji, usimulizi wa nafsi ya kwanza, usimulizi wa nafsi ya pili na usimulizi wa nafsi ya tatu.

Hivyo basi kwa kutumia *Utenzi wa Nabii Isa* tutabaini na kuangalia mbinu za usimulizi zinazojitikeza katika utenzi huu. Mwandishi wa *Utenzi wa Nabii Isa* kwa kiasi kikubwa ametumia usimulizi wa nafsi ya tatu. Wamitila, (ameshatajwa), anaeleza kuwa usimulizi wa nafsi ya tatu, ni usimulizi ambao hutambulishwa kwa na matumizi ya **ali-** , na kwambamsimuliziwa hadithi katika aina hii ya usimulizi hueleza matukio au mambo yanayohusu mtu mwingine. Pia tunaweza kusema ni aina ya usimulizi unaotumia viambishi awali “**a**” katika umoja na “**wa**” katika wingi. Viambishi hivi vimetumika sana katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Kwa mfano, ubeti (17 - 19),

17. **Walozidi** kwa imani,
Kumuamini Manani,
Bwana wetu Imrani,
Ndiye **aliyezidia**.

18. Bwana huyu muumini,
Mpendwa mno mjini,
Katika palestini,
Ndiko **alikoishia**.

19. **Alikuwa** huyu bwana,
Usiku hadi mchana,
Kimhofu Subuhana,
Thamma kumsujudia.

Aina nyingine ya usimulizi aliyotumia mtunzi ni usimulizi wa nafsi ya kwanza. Ni usimulizi ambao umejitokeza kwa kiasi kikubwa katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Huu ni usimulizi ambao unafanywa na mhusika kwa nafsi ya kwanza. Aidha mhusika anayetumia usimulizi wa nafsi ya kwanza hutumia viambishi vya nafsi ya kwanza. Kwa mfano, “**mimi**” na “**ni**”, “**si**” katika umoja na “**sisi**” na “**tu**” katika wingi. Usimulizi huu unaonekana katika mazungumzo mengi ya wahusika katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Kwa mfano:

129. Natubu kwako kiumbe,
Sikuja nikukurumbe,
Nimekuja na ujumbe,
Utokao kwa Jalia

131. Sikia nakwambia,
Sikufika kukutweza,
Nimekuja tekeleza,
Amri yake jalia.

132. **Menituma** Subuhana,
Mimi nawe kuonana,
Ili **nikupe** kijana,
Mtukufu kukujia.

Haya ni majibu ya mjumbe wa Mungu kwa Bi. Maryamu katika mazungumzo yao. Mtunzi amemsawiri mhusika katika mazungumzo ya nafsi ya kwanza, kuonyesha kwamba ni maneno yaliyotamkwa na mhusika mwenyewe. Viambishi vilivyokolezwa wino katika mfano wa hapo juu unaashiria dhana hii ya usimulizi wa nafsi ya kwanza.

Kwa upande mwingine, usimulizi maizi umepata nafasi katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Mohochi, (2000: 50) anaeleza kuwa usimulizi maizi hutokea pale ambapo mwandishi anaeleza hadithi ambayo yeye si mshiriki au haimhusu japo anaelewa mambo yote yanayoendelea na kutendeka katika hadithi nzima. Wamitila, (2003: 326) anaunga mkono mawazo ya Mohochi kwa kueleza kuwa, usimulizi maizi unamuonyesha msimulizi kuwa na ufahamu wa kila kitu katika hadithi. Anaongezea kusema kwamba, msimulizi maizi ana sifa ya ki-Ungu ya uwezo wa kupenya kwenye akili na mioyo ya wahusika wake na kueleza kile wanachowaza na kufikiri hata kabla hakijadhihirika kwa matendo. Usimulizi huu umejitokeza pale ambapo msimulizi anatueleza yaliyotamkwa na mtume Zakaria moyoni baada ya kujibiwa na Bi. Maryamu kuhusu vyakula anavyovipata kwake kila aendapo

kumzuru Bi. Maryamu. (ubeti 92, 97 na 98).Hapa msimulizi anaonyesha kufahamu anachokitamka Zakatia navile moyo wake ulivyoridhika kwa jibu alilopewa na Bi. Maryamu. Jambo ambalo Mungu pekee ndiye anao uwezo nalo.

Mtunzi wa *Utenzi wa Nabii Isa* pia ametumia usimulizi ngazi katika kuieleza hadithi yake. Wamitila, (ameshatajwa), anaeleza kuwa usimulizi ngazi ni usimulizi ambapo hadithi inategemezwa kwenye hadithi kuu ina vihadithi vingine vidogo vidogo. Huu ni mtindo wa usimulizi ambao umesheheni katika utenzi huu. Mfano katika *Utenzi wa Nabii Isa*, ni hadithi inayohusu maisha ya Nabii Isa mwenyewe. Hadithi hii ambayo ndiyo kuu imetegemezwa na hadithi nyingi ndogo ndogo. Hasa mwanzoni mwa utenzi wenyewe kabla ya hadithi kuu kusimuliwa tunapata hadithi ya maisha ya Bwana Imrani na mke wake ambayo inashikana na jinsi Bibi Maryamu ambaye ni mama yake Nabii Isa alivyopatikana na kuzaliwa. (ubeti17 – 55), kuna hadithi ya jinsi Bibi Maryamu alivyolelewa. Ni baada ya hadithi hii ndipo msimulizi anaianza hadithi yenyewe ya Nabii Isa. Pengine mtunzi anafanya hivi ili kutupa msingi mzuri wa kuielewa hadithi kuu. Aidha kwa kufahamu asili yake mhusika mkuu (Nabii Isa). Tutaelewa vema maisha yake na hivyo kuielewa vema hadithi yenyewe kwa ujumla.

4.4.2.2 Lugha

Kwa kawaida lugha ni nyenzo muhimu katika fasihi kwa sababu ndiyo itumiwayo kuwasilisha ujumbe. Ushairi ukiwa mojawapo wa tanzu za fasihi kadhalika, hutumia lugha katika kupitisha ujumbe. Lugha ya kishairi ni yenye mpangilio maalum wa maneno yaliyoteuliwa na mtunzi ili kuwasilisha ujumbe wake. Ni lugha inayovutia kwa kiasi kikubwa nadhari za hadhira yake mathalani, wasomaji na wasikilizaji wa mashairi. Si kwamba kuna lugha maalumu ya fasihi, chambilecho Wamitila, (2008: 68) bali mtunzi huchota lugha yake katika hazina pana na kuiajinabisha hivyo kuifanya ijitokeze kuwa tofauti na lugha ya kawaida. Mbinu hii ya uajinabishaji huhusishwa sana na ushairi ambao kutokana na kaida na kanuni za kimuundo lugha inayotumiwa huonekana tofauti na ile ya kawaida. Mbinu ambazo baadhi wa wataalamu wamezihusisha na lugha ya fasihi inayotokana na uajinabishaji wa lugha ni pamoja na tanakali za sauti, istiari, takriri, semi na kadhalika. Mbinu hizi zinapatikana katika *Utenzi wa Nabii Isa* kwa kiasi kidogo tu.

4.4.2.2.1 Tanakali za sauti

Tanakali za sauti ni mbinu ya kutumia maneno yanayoiga mlio au hali fulani au namna jambo hutendeka. Mbinu hii imetokea mara moja katika *Utenzi wa Nabii Isa* pale ambapo Nabii Isa alifanya muujiza wa kuumba ndege. Msimulizi anatumia mbinu hii kuiga sauti ya ndege hao ili kuonyesha kuwa walikuwa si vikaragosi alivyoumba Nabii Isa bali ni ndege halisi wenye uhai. (ubeti 472)

Hao nyuni wapakata,
Uhai watwetatweta,
Na pumzi wakivuta,
Chwi! Chwi! Chwi! Wajililia.

4.4.2.2.2 Tashbihi

Tashbihi ni mbinu inayotumiwa kufananisha vitu viwili au hali tofutikwa kutumia viunganishi kwa mfano “kama”, “ja”, “mithili ya” na kadhalika. Ni mbinu ambayo mtunzi ameitumia pia mara chache sana katika utenzi huu. Tashbihi tunazipata katika ubeti wa 312, 363, 706, 72

312 Kisha wanaiabudu,
Na kuwa kama wadudu,
Wajianisi kwa shudu,
Uvundo wajivunia.

363 Kwani Musa uhodari,
Mkono kituashiri,
Kofi lake huja nuri,
Anga kama shamsia.

Katika mifano tuliyotoa hapo juu ubeti wa 312, mtunzi anafananisha jinsi Wayahudi wanavyoabudu sanamu kwa wing na namna wadudu wanavyokusanyika wakati wanakula au wamevamia kitu. nayo tashbihi ya ubeti wa 363 mtunzi amefananisha nuru iangazayo itokayo katika mkono wa Nabii Musa alipofanya muujiza, kwamba hutoka nuru kama ya jua na kuangaza kote jinsi jua liangazavyo. Katika ubeti wa 706, mtunzi amefananisha namna ambavyo wanafunzi wa Nabii Isa walivyokula nyasi na ng’ombe walavyo wafuasi walipokosa chakula jangwani.

4.4.2.2.3 Takriri

Ni mbinu inayotumiwa na mtunzi kuisitiza jambo. Huitwa pia urudiaji. Takriri hutokea katika kazi ya fasihi katika daraja tofauti tofauti. Kwanza kuna takriri sauti ambayo inaweza kuwa irabu au konsonanti. Urudiaji huu unatupa aina mbili za takriri – takriri irabu au vokali na takriri konsonanti mtawalia. Mfano wa takriri irabu unatokea katika urari vina vya utenzi wote wa Nabii Isa. Kwa mfano ubeti wa 749 kina chake ni “a.” hivyo irabu a imerudiwa katika mishororo yote. Kwa upande mwingine takriri konsonanti tunaipata katika ubeti wa 693, ambapo komsonanti “s”ndiyo imeanza mitatu ya kwanza.

Daraja nyingine ya takriri inayodhihirika katika *Utenzi wa Nabii Isa* ni takriri neno. Huu ni urudiaji wa neno au maneno Katika utungo. Mtunzi anaweza kufanya hivi kwa kutilia mkazo jambo au hata kuchezea neno. Katika utenzi wa Nabii Isa tunapata takriri neno katika ubeti wa 10, msitari wa 2. Mtunzi anaposema “masanamu chungu chungu.” Kuonyesha wingi wa sanamu walizokuwa wakiabudu Wayahudi badala ya Mungu. Daraja nyingine ya takriri aliyotumia mtunzi ni ya takriri kifungu, ambayo tunaipata katika ubeti wa mwisho (834)Hapa mtunzi anamaliza dua yake na hali kadhalika utunzi wake kwa kutilia mkazo au kuisitiza heshima au kumuamini kwake Mungu aliyemuwezesha kutunga utenzi wake. Takriri ni mbinu ambayo mtunzi hajaishabikia sana.

Amina rabi amina,
Amina rabi amina,
Rabi wamaulidina,
Dua ninaishilia.

4.4.2.2.4 Sitiari

Wamitila, (2003: 202) anaeleza sitiari kuwa ni mbinu ya kulinganisha kitu kimoja na kingine ambayo haijitokezi waziwazi. Katika mbimu hii au ulinganisho huu hakuna matumizi ya viunganishi. Kama vile, “kama”, “ja”, na kadhalika. Japo “ni” au “kuwa” hutumika. Sitiari zinadhihirika katika Utenzi wa Nabii Isa katika ubeti wa 236 mshororo wa 3 mtunzi anasema mola wetu ni ngome. Katika sitiari hii mtunzi analinganisha Mungu nasifa ya ngome kuwa mahali pa kujihami dhidi ya maadui. Hivyo Nabii Isa anaposema Mungu ni ngome anamtuliza mama yake kwa kumhakikishia kuwa wana kinga imara dhidi ya maadui (watu wa jamaa yake) wanaomngoja kumshambulia kwa maneno makali na matusi. Nayo istiari

katika ubeti wa 266 mshororo wa 1. Inasema, mimi ni muanga. Hapa Nabii Isa anafananisha kazi yake ya kuongoza Waisraili na kuwaonyesha njia ya Mungu na mwanga unaomulika au kuangaza na kufanya watu waone vyema.

4.4.2.2.5 Tabaini

Tabaini ni mbinu ya usemi inayotumiwa kusesitiza ujumbe kwa kutumia maneno yanayokinzana au yanayokanushana. Katika *Utenzi wa Nabii Isa* mfano mzuri wa tabaini umetokea katika ubeti wa 693.

Si mfupi si mrefu,
Si mwembamba wa waswifu,
Si mnene kiarifu.
Umbo ukimwangalia.

4.4.2.2.6 Taniaba

Wamitila,(ameshatajwa, uk. 218), anaeleza taniaba kuwa ni mbinu ambapo mtunzi hutumia maelezo au sifa fulani au vivumishi fulani badala badala ya jina maalum. Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, mtunzi ametumia taniaba mara nyingi hasa kwa kumtaja Mungu. Amemuita Mungu muweza (ubeti 140, 153) kwa sifa ya kuwa na uwezo mkuu, Subuhana (ubeti 122, 132) kwa sifa ya kutakata na kila ovu na pia kutukuka, Jalia (ubeti 91) kwa sifa yake ya kufanya jambo liwezekane au kuwezesha, Rabana (119) kwa sifa yake ya ulezi, Karimu (ubeti 47, 109) kwa sifa yake ya ukarimu, Mwenyezi (ubeti 83) kwa sifa yake ya kuwa mwenye enzi yote na utukufu, Manani (ubeti 24) kwa sifa yake ya upaji na kadhalika.

4.4.2.3 Uhuru wa mtunzi

Mshairi ana uhuru wa kuifinyanga lugha kwa namna mbali mbali ilmradi afuate kanuni za utunzi. Anapofanya hivi, Mshairi anazua mbinu tofuti tofauti. Anaweza kuongeza silabi katika neno - mbinu inayoitwa mazida au kupunguza idadi ya silabi katika neno – mbinu inayoitwa inkisari. Aidha mshairi anaweza kubadilisha sauti katika neno - mbinu inayoitwa tabdila. Mtunzi hufanya hivi ili kupata urari wa vina au kusawazisha idadi ya silabi katika mshororo. Kadhalika mshairi anaweza kubadilisha maneno yasiyo ya Kiswahili yakatamkika kama ya Kiswahili – mbinu inayojulikana kama utohozi na hata kupanga maneno tofauti na mpangilio wa kisarufi. Hizi ni mbinu ambazo zimesheheni katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, inkisari imedhihirika sehemu nyingi. Kwa mfano, mtunzi

ametumia neno 'walozidi' badala ya waliozidi (ubeti 17), neno 'aloweka' badala ya aliyoweka (ubeti 35), neno 'babake' badala ya baba yake nakadhalika. Mtunzi alifanya hivi ilia pate idadi ya mizani inayotakikana katika kila mshororo.

Mbinu nyingine ni mazida ambayo imedhihirika katika beti tofauti tofauti katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Kwa mfano neno 'yuwamwandamia' badala ya 'yuwamwandama' (ubeti 115), neno 'waulizania' badala ya waulizana (ubeti 278), neno 'mursalia' badala ya 'mursali' (ubeti 592), na kadhalika. Hapa mtunzi ametumia mazida ili kupata urari wa vina. Kadhalika Mtunzi ametumia mbinu ya tabdila. Amefanya hivi ili kupata urari wa vina. Kwa mfano mtunzi ametumia neno 'Mariama' badala ya neno 'Mariamu' (ubeti 576, 602), neno 'wanaadama' badala ya 'wanaadamu' (ubeti 576), neno 'nuri' badala 'nuru' (ubeti 363) na kadhalika.

Mshairi vile vile anaweza kukiuka sheria za sarufi akapanga maneno tofauti. Katika *Utenzi wa Nabii Isa*, mbimu hii ni muhimu katika ushairi kwa sababu inasaidia kuleta urari wa vina hali kadhalika mdundo au mahadhi ya ushairi. Mtunzi anaweza akadondosha neno au hata kupanga maneno tofauti na vile yanapaswa kupangwa kisarufi. Katika *Utenzi wa Nabii Isa* mbinu hii inadhihirika katika kupangilia maneno tofauti na mpangilio wa kawaida wa kisarufi. Kwa mfano, ubeti 68 mshororo wa 1. **“kwa ajili sote sisi”** inapaswa kuwa **“kwa ajili sisi sote.”** Mtunzi amefanya hivi ili kupata urari wa vina katika ubeti huo ambao kina chake ni **si**. Mfano mwingine wa mbimu hii ni ubeti wa 85 mshororo wa 3. **“palo na waume mbali.”** Mpangilio sahihi wa mshororo huu ni **“palo mbali na waume”** kadhalika mpangilio huu umefanyika ili kupata urariwa vina vya ubeti huu ambacho ni **“li.”**

2.5 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili maudhui na muundo wa *Utenzi wa Nabii Isa*. Jambo hili limetusaidia kuufahamu na kuuelewa vyema utenzi huu. Kwa kuuelewa vema *Utenzi wa Nabii Isa* utatusaidia kujadili mada ya utafiti wetu. Aidha mitindo mbali mbali ambayo mtunzi wa *Utenzi wa Nabii Isa* ametumia. Mpangilio wa matukio yanayojitokeza katika utenzi huu na jinsi yalivyopangwa yatatuwezesha kuhakiki kipengee cha wakati katika utenzi huu. Aidha muundo wake uliosaili utasaidia kuuhakiki utenzi huu kufuatia mada iliyoteuliwa.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MAHITIMISHO, NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika tasnifu hii tumeshughulikia usimulizi katika *Utenzi wa Nabii Isa* ukiongozwa na nadharia ya naratolojia. Dhamira yake ikiwa ni kutathmini usimulizi katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Aidha ulinua kubainisha vipengee ya usimulizi na dhima ya vipengee hivi katika hadithi kwenye *Utenzi wa Nabii Isa*. Kadhalika sura hii inatoa muhtasari wa utafiti na vile vile kutoa mapendekezo kuhusu suala la usimulizi katika tenzi hususan *Utenzi wa Nabii Isa*. Aidha kufafanua iwapo malengo yameafikiwa au la. Tumechanganu vipengee vya usimulizi vya wakati na uwasilishaji usemi. Katika utafiti wetu tumetambua kwamba usimulizi ni dhana pana sana. Kadhalika tumegundua kwamba mtunzi wa *Utenzi wa Nabii Isa* ametumia kiasi kikubwa cha vipengee vya usimulizi vilivyoteuliwa kuhakikiwa katika utafiti huu. Aidha tumejadili mambo ya kimsingi ya *Utenzi wa Nabii Isa* mathalani, muundo, mtindo na maudhui.

5.2 Matokeo ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengomnneambayo ulinua kuyatathmini. Hapo awali tulikuwa tumechukulia kwamba kwa sababu usimulizi huhusishwa na tungo za kinathari, basi hauna nafasi katika utenzi na hususan *Utenzi wa Nabii Isa*. Katika uchanganuzi wetu tumetambua kwamba vipengee vya usimulizi vimetumika katika hadithi ya au kisa cha Nabii Isa na kwamba vina dhima kubwa katika uelewekaji wa hadithi yenyewe na kupitisha ujumbe katika hadithi mathalani, maudhui katika hadithi, kwa mfano katika *Utenzi wa Nabii Isa* maudhui ya usaliti, ndoa, malezi na maadili miongoni mwa mengine yamepitishwa.

Katika kipengee cha wakati utafiti huu umebaini kuwa kipengee cha mpangilio wa matukio katika *Utenzi wa Nabii Isa* hakijatumika kikamilifu kwa sababu mtunzi ametumia sana aina moja ya mpangilio ambayo ni analepsia kuliko ya prolepsia. Hata hivyo tumeweza kujua matukio ya nyuma katika hadithi ambayo yanatupa habari muhimu katika uelewekaji wa

hadithi na hasa kumuelewa mhusika anayelengwa katika hadithi. Aidha inatupa mwelekeo wa matukio katika hadithi.

Muda pia umejadiliwa katika utafiti huu kwa kuvichunguza vipengee vyake ambavyo ni; mtuo, onyesho, muhtasari na udondoshi. Matumizi ya vipengee hivi hupunguza na kuathiri wizani wa hadithi hii ya Nabii Isa. Kwa mfano muhtasari huleta kasi ya juu katika simulizi ilhali mtuo huleta kasi ya chini. Dhana hizi mbili hutofautiana katika mawanda na kusababisha kutofautiana kwa wizani katika simulizi. Umara au idadi marudio ni kipengee kingine cha wakati ambacho pia kimejadiliwa katika utafiti huu. Mtunzi wa *Utenzi wa Nabii Isa* ameonyesha matumizi ya umara katika hadithi hii ya Nabii Isa. Aina za idadi marudio zilizotumika ni pamoja na usimulizi banifu, usimulizi rudufu na usimulizi mosi.

Kipengee kingine cha usimulizi kilichojadiliwa ni kipengee cha uwasilishaji usemi. Katika utafiti wetu tumeonyesha kwamba uwasilishaji usemi ni mbinu mojawapo ambayo imetumika katika kueleza ujumbe katika *Utenzi wa Nabii Isa*. Mbinu za uwasilishaji usemi ambazo zimedhihirika katika *Utenzi wa Nabii Isa* ni kama vile; usemi halisi na mawazo halisi, usemi wa taarifa na mawazo taarifa, usemi halisi huru na mawazo halisi huru na usemi taarifa huru. Mawazo taarifa huru ni mbinu ambayo haijadhihirika katika *Utenzi wa Nabii Isa*.

Mwisho kabisa umetambua kwambavipengee anuai vya usimulizi vimedhihirika katika utenzi huu wa Nabii Isa. Hivyo basi kwa kudhihirika kwa vipengee hivi ni wazi kwamba mtunzi wa *Utenzi wa Nabii Isa* amefaulisha uelewekaji wa utenzi huu. Ambapo katika naratolojia, muhimu katika simulizi si usomaji na ufasiri wa hadithi bali uelewekaji wa hadidhi yenyewe na jinsi hadithi yenyewe ilivyotungwa kwa kuzingatia vipengee tofauti tofauti vya usimulizi.

5.3 Mapendekezo

Kwa sababu ya upana wa suala la usimulizi, ni vigumu utafiti kuchunguza suala hili kwa mapana. Utafiti huu umechunguza vipengee viwili tu vya usimulizi katika *Utenzi wa Nabii Isa* ambavyo ni wakati na uwasilishaji usemi. Hivyo tunapendekeza kwamba tafiti za baadaye zichunguze vipengee vingine vya usimulizi na hata dhana nyingine zinazohusiana na

usimulizi ambazo hazijajadiliwa katika utafiti huu, kama vile mtazamo, daraja za sauti, wahusika na uhusika, usimulizi, na nyinginezo.

Kadhalika tunapendekeza kwamba tafiti za baadaye zichunguze usimulizi katika tungo nyingine za tenzi za Kiswahili ilikukuza na kuimarisha fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu Vile vile unapendekeza tafiti zijazo katika *Utenzi wa Nabii Isaziongozwe* na nadharia nyingine kama vile mwingiliano matini wa *Utenzi wa Nabii Isa* na maisha ya Yesu Kristu katika Biblia Takatifu na nadharia nyinginezo.

MAREJELEO

- Abedi, K. A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Arege, T. (2012). *Narration in Kiswahili Narrative Poetry: An Analysis of Utenzi wa Rasi Ighuli*. Chuo Kikuu cha Nairobi (haijachapishwa).
- Barry, P. (1993). *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory*. Manchester: Manchester University Press.
- Barry, P. (1995). *Beginning Theory*. New York: Manchester University Press.
- Barry, P. (2000). *Beginning Theory*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Brogan, A. P. (Ed.). (1993). *The New Princeton Encyclopedia of Poetry and Poetics*. Princeton, New Jersey: Princeton University Press.
- Burundi, W. n. (2014). Usimulizi katika Utenzi wa Swafiya na Nguvu Malikatika Kioo cha Lugha. *Jarida la TATAKI*, 12, 74.
- Fielder, G. E. (1995). Narrative Perspective and The Bulgarian L - Participle. *Slavic and East European Journal*, 585 - 600.
- Forster, M. E. (1927). *Aspects of The Novel*. London: Penguin Books.
- G., S. O. (Ed.). (1996). *Narratology: An Introduction*. New York: Longman Publishers.
- Gathira, F. K. (2013). *Taswira ya Jagina katika Utend: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Nabii Isa*.
- Genette, G. (1980). *Narrative Discourse; An Essay in Method*. Ithaca New York: Cornell University Press.
- Rimmon-Kenan, S. (1983). *Narrative Fiction Contemporary Poetics*. London: Routledge.
- Landa, J. A. (1990). *Narrative Theory*. University of Zaragoza.
- M'ngaruthi, K. T. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mohamed, S. (1995). *Kunga za Nadharia ya Kiswahili*. Nairobi: EAEP.
- Mohochi, E. (2000). usimulizi wa Riwaya ya Nyongo Mkalia Ini. *Nordic Journal of African Studies*, 9, 50.

- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Indiana University: EAEP.
- Mulama, S. J. (2011). *Usimulizi Katika Utenzi wa Siri Li Airali*. University of Nairobi.
- Mzenga, M. (1977). *Utenzi wa Nabii Isa*. Nairobi: Foundation Books.
- Ong'ondi, B. E. (2005). *Uhakiki wa Maudhui Teule katika Utenzi wa Nabii Isa*. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Ong'ondi, B. E. (2005). *Uhakiki wa Usimulizi Katika Riwaya ya Walenisi*. chuo Kikuu cha Nairobi.
- Ouma, O. K. (2005). *Uhakiki wa Maudhui Teule Katika Utenzi wa Nabii Isa*. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Prince, G. (1982). *Narratology: The Form and Functioning of Narrative*. New York, Amsterdam, Berlin: Mouton Publishers.
- Rimmon-Kenan, S. (2002). *Narrative Fiction Contemporary Poetics*. London: Routledge and Co. Ltd.
- TUKI. (2006). *English - Kiswahili Dictionary*. Institute of Kiswahili Research. University of Dar es Salam.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengee Vyake*. Nairobi: Focus Publishers (K) Ltd.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books Publications Ltd.
- Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi*. Nairobi: Vide - Muwa Publishers Ltd.
- Wenzake, B. n. (2014). Usimulizi katika Utenzi wa Swafiya na Nguvu Mali katika Kioo cha Lugha. *Jarida la TATAKI*, Juzuu 12.
- Wolf, W. (2002). *Current Trends in Narratology*. Austria: University of Graz.